**Mghwira** azikwa Arusha, serikali yamuenzi kwa kumjengea barabara

UKURASA 7



**Wastaafu** watarajiwa wapewa angalizo dhidi ya matapeli wa mafao

UKURASA 8




UKURASA 11


# Nipashe

Jumanne Julai 27, 2021 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-

MWANGA WA JAMII

ISSN 0856 • Na. 0580654

www.ippmedia.com

www.twitter.com/nipashetz

www.facebook.com/nipashetz

www.instagram.com/theguardian_newspaper

LIKE & FOLLOW US


# Mbowe kortini kimyakimya Dar



## **ASHTAKIWA** kwa ugaidi, adaiwa mgonjwa, wanachama waibuka... *Endelea ukurasa 2*



Abiria wakipanda gari kwa kugombania huku wakiwa hawajachukua hatua za kujikinga na ugonjwa wa corona katika kituo cha mabasi Mnazi Mmoja jijini Dar es Salaam jana. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# RC Dar aagiza 'level seat', Dodoma yazalisha oksijeni

UKURASA 2&3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### ANAYEDAIWA KUMTEKA MO AACHIWA HURU

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemwachia huru dereva teksi, Mousa Twaleb, aliyekuwa akidaiwa kushiriki kumteka Mohammed Dewji (MO)...

UKURASA WA 16

### JELA MIAKA MINNE KUUA MPENZI BILA KUKUSUDIA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imemhukumu kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka minne jela binti wa miaka 19 baada ya kupatikana na hatia ya kumuua bila kukusudia...

## Shahidi aeleza alivyopigwa, kuteswa na Ole Sabaya

UKURASA 5

**MICHEZO** **SIMBA YAIPIGA YANGA KIJEMBE** UK.24 **MAONI, KATUNI** UK.6

## HABARI KITAIFA

# Mbowe kortini kimyakimya

**Na Waandishi Wetu**

MWENYEKITI wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA), Freeman Mbowe, jana alifikishwa Mahakama ya Hakimu Mkazi Kisutu jijini Dar es Salaam, na kusomewa mashtaka ya ugaidi.

Taarifa iliyotolewa na Mkurugenzi wa Itifaki, Mawasiliano na Mambo ya Nje wa chama hicho, John Mrema, ilieleza kuwa mwenyekiti huyo alifikishwa katika mahakama hiyo kimyakimya pasipo kuwa na uwakilishi wa wanasheria wa chama wala familia.

Mbowe alikamatwa na Jeshi la Polisi mkoani Mwanza wiki iliyopita akiwa hotelini akijiandaa kufanya kongamano la kudai Katiba mpya na baadaye alisafirishwa hadi jijini Dar es Salaam kwa mahojiano kwa makosa aliyokuwa akituhumiwa.

Msemaji wa Jeshi la Polisi, David Misime, alieleza kwamba Mbowe anakabiliwa na makosa ya ugaidi ya kupanga njama za kuua viongozi wa serikali.

**MBOWE ADAIWA KUUGUA**

Jana, CHADEMA kupitia kwa Mrema, ilieleza kwamba ilipokea taarifa kutoka kwa wanafamilia wa Mbowe ambao walimtembelea Kituo cha Polisi Oysterbay alikokuwa ameshikiliwa, wakieleza kuwa Mbowe anaumwa, lakini Jeshi la Polisi halijampeleka hospitali.

Mrema alisema wana ndugu hao walimtembelea Mbowe jana asubuhi na kupata taarifa kuwa anaumwa, lakini hadi saa sita mchana ya siku hiyo alikuwa bado hajapelekwa hospitali kwa ajili ya vipimo na matibabu.

"Chama kimewaelekeza mawakili wake kufika mara moja kituo cha polisi Oysterbay kwa ajili ya kumuona Mwenyekiti. Tunalitaka Jeshi la Polisi limpeleke hospitali mara moja, kwani ni haki ya mtuhumiwa kupatiwa matibabu kwa mujibu wa sheria za Tanzania," alisema Mrema.

Kamanda wa Polisi Kanda Maalum ya Dar es Salaam, Jumanne Muliro, alipoulizwa, alisema: "Ukikaa ukasema ninaumwa nipeleke hospitali na tunakuona mzima na tuna madaktari wa polisi, sisi tunazungushwa na mtuhumiwa?"

Kamanda Muliro alisema Kituo cha Polisi Oysterbay kuna hospitali na wapo madaktari wa jeshi ambao hutembelea mahabusu kuangalia wagonjwa.

"Kwa hiyo siyo suala la kusema mimi nipelekwe hospitali, si unajua mbinu za watuhumiwa...kama unaumwa tutakupeleka hospitali, lakini siyo kama wewe unavyotaka, vinginevyo watuhumiwa wote tungekuwa tunawasikiliza wanavyotaka ungekuta wamekaa vitandani Muhimbili na wengine Mwananyamala wamejilalia tu wanasema wanaumwa," alisema Kamanda Muliro.

**MAWAKILI KWENDA KORTINI LEO**

Upande wa utetezi katika kesi inayomkabili Mbowe, ulieleza kuwa unatarajiwa kwenda Mahakama Kuu leo kufungua maombi ya kupinga hati ya mashtaka hayo.

Akizungumza na Nipashe nje ya mahakama, Wakili Peter Kibatala, alisema watawasilisha maombi Mahakama Kuu Kanda ya Dar es Salaam kupinga uhalali wa hati ya mashtaka dhidi ya Mbowe.

"Pia, hati ya mashtaka ina upungufu wa kisheria, tunakwenda kuomba Mahakama Kuu ifanye marejeo na kuona uhalali wa hati hiyo kuwapo mahakamani," alisema Kibatala.

Wakati huo huo, viongozi wa CHADEMA Kanda ya Pwani wakiongozwa na Mkuu wa Kitengo cha IT wa Kanda hiyo, Mackdeo Shilinde, akizungumza na waandishi wa habari jana walisema hawaridhishwi na mwenendo wa mwenyekiti wao, Freeman Mbowe.

Walielezwa kuchukizwa na namna mwenyekiti wao anavyoongoza chama hicho kwa maamuzi binafsi, ambayo yanakwenda kinyume na katiba ya chama.

Viongozi hao wameeleza baadhi ya mapungufu yaliyo kwenye katiba ya chama hicho ambayo yamekuwa sababu ya CHADEMA kukosa wanachama na wawakilishi katika ngazi ya mitaa na misingi, Pia wamesema mapungufu hayo yanampa mwanya Mbowe kuwa mwenyekiti wa kudumu wa chama hicho.

Kuhusu katiba mpya, Shilinde alidai katiba ya chama chao bado ina mapungufu ambayo yanapaswa kufanyiwa kazi kabla ya chama hicho kuelekeza nguvu zake katika kudai katiba mpya.

Shilinde alieleza malengo ya CHADEMA hayakuwa ya kudai katiba mpya bali ilikuwa ni kukiimarisha chama katika ngazi ya misingi, ili kujiweka katika mazingira mazuri ya kupata ushindi kwenye chaguzi zijazo.

Mwenyekiti wa CHADEMA Wilaya ya Temeke, Martin Karugendo, alihoji: "Kama CHADEMA hatuna viongozi katika ngazi ya mitaa na hatuna wabunge, hata wakipiga kelele kuhusu madai ya Katiba Mpya katika mitandao ya kijamii, nani atapitisha katiba hiyo bungeni?"

Alidai wao kama wanachama wa CHADEMA wanatamani kuona chama chao kikijikita katika kujiimarisha ili kupata matokeo mazuri katika uchaguzi mkuu wa urais mwaka 2025 na wabunge.

***Imeandikwa na Romana Mallya na Hellen Mwango***

# Mpango atoa agizo Bandari ya Mtwara

**Na Mary Geoffrey**

MAKAMU wa Rais, Dk. Philip Mpango, ameiagiza Wizara ya Kilimo, kuhakikisha mazao yanayotoka ukanda wa kusini pamoja na viuatilifu vyote vinavyotumika kwenye mazao ya korosho vinasafirishwa kwa kutumia Bandari ya Mtwara.

Dk. Mpango alitoa agizo hilo, jana mkoani humo alipotembelea Bandari ya Mtwara, ikiwa ni mwendelezo wa ziara yake ya siku tano mkoani humo.

Akiwa mkoani humo, Dk. Mpango alisema Bandari ya Mtwara ni hazina kubwa ambayo serikali imewekeza fedha nyingi, hivyo itumike vizuri ili Watanzania wanufaike na uwekezaji huo mkubwa.

Aidha, aliitaka Mamlaka ya Bandari (TPA), kuhakikisha inapunguza malalamiko ya wateja kwa kuimarisha ubora wa huduma wanazozitoa ikiwa ni pamoja na kusimamia usalama wa mali zao.

"Watumishi wa Bandari mna dhamana kubwa ya kusimamia ubora wa huduma mnazozitoa pamoja na kuhakikisha mnatafuta masoko ndani na nje ya nchi ili kutangaza bandari hii," alisema Dk. Mpango.


## TANGAZO LA MNADA / NOTISI / TAARIFA

**MALAPA AUCTION MART CO LTD** KWA NIABA YA **CRDB BANK PLC** TUNATOA NOTISI YA SIKU 14 TANGAZO NA TAARIFA KWA WAMILIKI WA DHAMANA ZIFUATAZO WAWE WAMELIPA MADENI YAO YOTE YA CRDB PAMOJA NA GHARAMA ZA DALALI VINGINEVYO TUTAUZA DHAMANA ZAO KWA MNADA WA HADHARA ILI KUFIDIA MADENI YAO.

| NA | MMILIKI/ MDHAMINI | DHAMANA | USAJILI | MAHALI ILIPO | TAREHE / SAA YA MNADA |
|---|---|---|---|---|---|
| 1 | DAUDI GABRIEL SANGA | NYUMBA | HATI YA MAUZIANO | MBEYA MJINI | 18/8/2021 KUANZIA SAA 6 MCHANA |
| 2 | MENAS MASENGO | NYUMBA | TITTLE 42032 LO. 142461 | IRINGA MJINI | 20/8/2021 KUANZIA SAA 6 MCHANA |
| 3 | MATHIAS PASCAL MASANJA | NYUMBA | HATI YAMAUZIANO | MANYONI PLOT NO. 1052 BLOCK AA | 22/8/2021 KUANZIA SAA 6 MCHANA |
| 4 | WILLIAM GRATION KALIKAWE | NYUMBA | TITTLE 14715 LO 161583 | KONGWA–DODOMA PLOT NO. 209 BLOCK D | 23/8/2021 KUANZIA SAA 6 MCHANA |
| 5 | AHMED MUSSA KIDUKA | NYUMBA | TITTLE 14214 LO 161164 | KONDOA–DODOMA PLOT NO 91 BLOCK BB | 24/8/2021 KUANZIA SAA 6 MCHANA |

### MASHARTI YA MNADA

1. MNADA UTAFANYIKA SEHEMU DHAMANA ILIPO.
2. MNUNUZI ATALAZIMIKA KULIPA 25% YA BEI PAPO HAPO NA 75% NDANI YA SIKU 14 BAADA YA MNADA.
3. ENDAPO MTEJA ATASHINDWA KULIPA NDANI YA SIKU 14 KIASI KILICHOLIPWA AWALI HAKITARUDISHWA NA MNADA UTARUDIWA.
4. GHARAMA ZA KUBADILI HATI MILIKI NI JUU YA MNUNUZI MWENYEWE.

### TAARIFA

MINADA YOTE ILIYOTANGAZWA TAREHE **17JULAI 2021** KATIKA GAZETI LA NIPASHE ITAFANYIKA KUANZIA SAA 6 MCHANA NA KUENDELEA.

216374002

KWA MAWASILIANO;
PIGA SIMU
0713 604044 / 0688 686905
0763 839700 / 0759 833833


# RC Dar aagiza 'level seat'

**Na Mary Geoffrey**

MKUU wa Mkoa wa Dar es Salaam, Amos Makalla, amepiga marufuku watu kujaa kwenye vyombo vya usafiri (daladala), abiria wote kuhakikisha wanavaa barakoa ili kujikinga na ugonjwa wa corona.

Pia, ameziagiza kamati za ulinzi na usalama za wilaya kusimamia utekelezaji wa mwongozo wa Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto, kuhusu kuchukua tahadhari dhidi ya ugonjwa huo.

Alitoa agizo hilo jana ikiwa ni siku moja tangu Wizara ya Afya, itoe mwongozo wa namna ya kujikinga na ugonjwa huo.

Makalla alipiga marufuku watu kuingia katika vyombo vya usafiri bila kuvaa barakoa na kujazana na kuiagiza Mamlaka ya Udhibiti wa Usafirishaji Nchi Kavu (LATRA) kusimamia utekelezaji wake.

Kadhalika, alipiga marufuku watu kukusanyika sehemu za kutolea huduma bila kuvaa barakoa.

Makalla alisema serikali imejipanga kutoa huduma bora za matibabu kwa wagonjwa wote watakaofika hospitali na kuwataka wananchi watakaoona dalili za ugonjwa wa virusi vya corona kuwahi kituo cha afya.

Wakati serikali ikitoa angalizo hilo, Nipashe lilipita katika baadhi ya maeneo ya mikusanyiko ya watu na kukuta wameendelea kuwapo bila kuvaa barakoa wala kuchukua tahadhari.

Nipashe lilishuhudia abiria wakiwa wanaendelea kujazana kwenye daladala na vituoni vya mabasi bila kuwa na barakoa.

Katika maeneo ya masoko wananchi waliendelea na shughuli zao kama kawaida bila kuzingatia mwongozo uliotolea na serikali.

Baadhi ya wananchi katika kituo cha daladala cha Makumbusho, walilieleza Nipashe kuwa hawajavaa barakoa kwa sababu hawaoni kama ugonjwa huo ni tishio.

"Wanakufa wenye hela huko, sisi maskini tunaozurura juani kuanzia asubuhi hadi usiku huyo corona anakaa wapi," alihoji Jumanne Issa.

Naye mfanyabiashara katika kituo hicho, Mwanaisha Rashid, alisema kuwa watu hawachukui tahadhari kwa sababu ya mazingira na shughuli wanazofanya.

"Tahadhari wanachukua wanaokaa maofisini sisi huku tupo juani muda wote lakini kujizipa pua na mdomo katika mkusanyiko mkubwa kwa muda mrefu ni hatari, tunachoamini Mungu anatulinda," alisema Mwanaisha.

Naye Mariam Yusuph alisema elimu bado inahitajika kwa sababu kunachowafanya watu wasivae barakoa ni mazoea na kujiaminisha uongo.

Alisema watu wanaona ni kawaida tu na hawajalichukulia hili suala la ugonjwa wa corona kwa uzito na hata uvaaji wa barakoa limekuwa suala la mtu binafsi zaidi.

Juzi, Katibu Mkuu wa Wizara ya Afya, Prof. Abel Makubi, alitangaza mwongozo mpya wa ugonjwa wa virusi vya corona pamoja na mambo mengine umepiga marufuku mikusanyiko ikiwamo ya kisiasa na kidini.

Prof. Makubi alisema pamoja na mambo mengine, mwongozo huo umelenga kukata mnyororo wa maambukizi katika ngazi ya kaya na jamii bila kuathiri shughuli za kiuchumi.

HABARI KITAIFA

# Hospitali Dodoma yaanza kuzalisha Oksijeni

**Na Paul Mabeja,** DODOMA

KATIKA kukabiliana na uhitaji mkubwa wa hewa ya Oksijeni katika hospitali mbalimbali nchini, Hospitali ya Rufani ya Mkoa wa Dodoma imeanza kufua hewa hiyo na kwa siku ina uwezo wa kuzalisha kati ya mitungi 250 hadi 300.

Mganga Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Best Magoma, aliyasema hayo juzi wakati alipotembelea hospitali hiyo akiwa na Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka.

Alisema pamoja na kuzalisha kiasi hicho cha hewa pia wamesambaza mtandao wa hewa hiyo kutumia mabomba katika wodi ya watoto, upasuajii na ya wagonjwa mahututi (ICU).

Alisema hewa hiyo pamoja na kutumiwa na wahitaji wengine kama vile majeruhi wa ajali, pia itakuwa ni sehemu ya kuchukua tahadhari ya kujilinda na mlipuko wa virusi vya corona wimbi la tatu kama itatokea uwapo wa wagonjwqa wengi katika hospitali hiyo.

"Uzalishaji huu umepunguza gharama za ununuzi wa hewa katika hospitali hii kwasababu si ya kununua ni ya kutengenezwa mmejionea pia vitanda vingi vitupu ni moja ya maandalizi ya kipindi hiki cha Uviko-19," alisema. Mganga Mfawidhi wa Hospitali ya Rufani ya Dodoma, Dk. Ernest Ibenzi, alisema hewa hiyo inayozalishwa inaweza kuhudumia watu 200 kwa mara moja.

"Toka tuanze kuzalisha hewa hii bado hatujawahi kufikisha idadi hiyo," alisema.

Alisema kuwa kwa mara ya mwisho kupata wagonjwa wengi wanaohitaji hewa ya Oksijeni ilikuwa ni wagonjwa 29 pekee kwa wakati mmoja.

Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Mtaka akizungumza katika ziara hiyo aliwataka wananchi wanaokwenda kuwaona wagonjwa katika hospitali hizo kuhakikisha wanavaa barakoa ili kujikinga wao na wagonjwa.

Alisema ni marufuku kwa mtu yeyote anayekwenda kumuona mgonjwa au kupelekea chakula kuruhusiwa kuingia kama hajavaa barakoa.

"Mganga Mkuu wa Mkoa amesema kuwa wanaokwenda kumwona mgonjwa wasizidi watu watatu, sisi wa mkoa tumeyapokea, lakini nyongeza yake ni ukitaka kwenda kumuona mgonjwa, kumpelekea chakula bila kuvaa barakoa hatutakuruhusu, ili uruhusiwe kumuona kwenye zahanati, kituo cha afya, hospitali ya serikali au ya binafsi tunawaomba mvae barakoa kwa faida yako na mgonjwa pia," alisisitiza Mtaka.

Aliwashauri watu wote wanaojihisi kuwa na dalili za ugonjwa wa corona wasibahatishe kuhusu tiba bali waende kwenye zahanati, vituo vya afya na hospitali kupimwa ili kuwa na uhakika.

Vile vile, alizitaka daladala kupakia 'level seat' na bodaboda kuzingatia sheria ya kupakia abiria mmoja ili kuepukana na maambukizi ya ugonjwa huo.

Alikiri uwapo wa wagonjwa wa corona mkoani hapo na kudai kuwa mkoa bado wanajitosheleza kuwahudumia kwa vile hakuna idadi kubwa ya wagonjwa.



Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Tanzania, Dayosisi ya Meru, Dk. Elias Kitoi akiuombea mwili wa marehemu aliyekuwa Mkuu wa Mkoa mstaafu wa Kilimanjaro, Anna Mghwira, wakati wa ibada ya maziko katika Kijiji cha Manyata wilayani Arumeru jana. **PICHA: CYNTHIA MWILOLEZI**

# Anayedaiwa kumteka MO aachiwa huru

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Kisutu imemwachia huru dereva taksi, Mousa Twaleb, aliyekuwa akidaiwa kushiriki kumteka Mohammed Dewji (MO).

Twaleb ameachiwa huru jana mbele ya Hakimu Mkazi Mkuu, Huruma Shaidi baada ya Mkurugenzi wa Mashtaka nchini kuwasilisha hati akionyesha hana nia ya kuendelea na shauri hilo.

Wakili wa Serikali, Esther Martin, alidai kwamba shauri hilo lilikuja kwa ajili ya kutajwa, lakini DPP amewasilisha hati, Jamhuri haina nia ya kuendelea na shauri hilo.

Mahakama ilikubali maombi ya Jamhuri na kumwachia huru mshtakiwa huyo ambaye alikuwa mahabusu gerezani tangu mwaka 2018.

Juni mwaka huu, Hakimu Shaidi alisema shauri hilo la muda mrefu na alikuwa haridhishwi na mwenendo wake.

"Nimefikisha kesi hii mbele ya wahusika akiwamo mwakilishi wa DPP, mshtakiwa kama ana kosa aendelee kushtakiwa kwa kosa lake au apewe dhamana ya polisi wakati akisubiri washtakiwa wengine wakamatwe.

"Nimelipendekeza hili shauri la muda mrefu na mwelekeo wake siuelewi," alisema Hakimu Shaidi.

Watuhumiwa wengine ambao upande wa mashtaka ulikuwa unawatafuta ni raia wanne wa Msumbiji na mmoja wa Afrika Kusini wanaodaiwa kumteka mfanyabiashara huyo.

Washtakiwa hao ni Phila Tshabalala raia wa Afrika Kusini, Henrique Simbine, Daniel Manchice, Issac Tomo na Zacarious Junior wote raia wa Msumbiji.

Katika kesi hiyo inadaiwa Mei Mosi na Oktoba 10, 2018, katika maeneo ya jiji la Dar es Salaam na Johannesburg Afrika Kusini, kwa makusudi washtakiwa wote kwa pamoja waliendesha genge la uhalifu.

Pia inadaiwa Oktoba 11, 2018 maeneo Hoteli ya Colloseum, wilayani Kinondoni Dar es Salaam, Twaleb pamoja na watu wengine ambao hawapo mahakamani, walimteka nyara MO kwa nia ya kumuhifadhi kwa siri na kumuweka maeneo ambayo ni hatari.

Inadaiwa Julai 10, 2018 maeneo ya Mbezi Beach wilayani Kinondoni, Dar es Salaam, Twaleb alitakatisha Sh. 8,000,000 wakati akijua fedha hizo ni zao la kosa la kushiriki genge la uhalifu.

MO alitekwa nyara Oktoba 11, mwaka 2018 alfajiri maeneo ya Hoteli ya Colloseum wakati akienda kufanya mazoezi na alipatikana Oktoba 20, mwaka huo huo katika eneo la Gymkhana.


**ABBOTT FUND TANZANIA LIMITED**
**(Certificate of Compliance No. 1828)**

**PUBLIC NOTICE MADE PURSUANT TO REGULATION 13 (A) OF THE NON GOVERNMENTAL ORGANISATION ACT**

**(AMENDMENTS) REGULATIONS 2018 MADE UNDER GOVERNMENT NOTICE NO. 609 OF 19TH OCTOBER 2018**

**WHEREAS** Regulation 13 (a) of the abovementioned regulations require that all non-governmental organisations in Tanzania publish bi annually funds received and their expenditure in a widely circulated newspaper which are accessible by the targeted beneficiaries as part of financial transparency and accountability compliance requirements.

**IN VIEW OF THE ABOVE,** we wish to make the following public disclosure of the funds approved for 2021 activities and their proposed expenditure, which publication covers the reporting period from
**1st July, 2021 to 31st December, 2021:**

| Project Area Expenditure | Amount in (USD) |
|---|---|
| **Muhimbili National Hospital Sustainability Strategy Support:** Includes support to Emergency Medicine; Central Pathology Laboratories; Leadership Capacity-Building | 500,000 |
| **Emergency Medicine Regional Amplification:** Includes Infrastructure project at Dodoma Regional Referral Hospital | 750,000 |
| **Building Livelihoods:** Includes National Children's Centre Infrastructure Project (Dodoma) | 375,000 |
| **Administration:** Includes travel, office costs and program implementation staff | 1,785,000 |
| Total Funds | **3,410,000** |

**ISSUED BY**
**EXECUTIVE DIRECTOR**
**ABBOTT FUND TANZANIA LIMITED**

216373602

MAKALA MAALUMU

# Mauaji wivu wa mapenzi yanavyoacha simanzi -2

## Polisi, LHRC na wanasaikolojia wanena

**Na Maulid Mmbaga**



**SEHEMU ya kwanza ya ripoti hii, iliangazia idadi ya matukio ya mauaji, na ilionyesha sababu ni wivu wa mapenzi ambao ulikuwa na jumla ya matukio 38, kwa kipindi cha Juni mwaka 2020 hadi Julai 2021. Endelea...**

Agosti 8, Jeshi la Polisi mkoani Kagera lilimshikilia Ayoub John (38), kwa tuhuma za kumuua kwa kumchinja mtoto wake wa kambo Aidan Greyson (3), chanzo wivu wa kimapenzi.

Siku hiyo hiyo, Polisi mkoani Pwani lilimshikilia mwalimu wa Shule ya Msingi Mwendapole, Evata Mboya (50), kwa tuhuma za kumtandika mwanafunzi aliyepiga kelele

Agosti 12, Jeshi la Polisi mkoani Rukwa, liliripoti kumsaka Joseph Kalolo, kwa tuhuma za kumuua mkewe kwa kumnyonga kwa wivu wa mapenzi.

Agosti 13, Jeshi la Polisi mkoani Morogoro, lilimshikilia Shinje Njilangila (30), mkazi wa Kilosa kwa tuhuma za kumuua shemeji yake Dotto Ngembe (28), kwa kumchoma na kitu chenye ncha kali sababu ni wivu wa kimapenzi. Agosti 17, mwalimu wa Shule ya Tumbatu mkoa wa Kaskazini Unguja, Hamadi Mdungi (36), alifikisha mahakamani kwa tuhuma za kumtorosha mwanafunzi mwenye umri wa miaka 14 akiwa chini ya uangalizi wa wazazi wake na kumbaka.

Agisti 19, Jeshi la Polisi mkoani Shinyanga, lilimshikilia Paschal Coloneli (27) kwa tuhuma za kumpa mimba mtoto wa darasa la tano.

Agosti 20, Mahakama ya Wilaya ya Lindi, ilimhukumu Maulidi Salum (25) mkazi wa kata ya Nangosa, kifungo cha miaka 30 jela, kuchapwa viboko 12, na kulipa milioni 2, baada ya kukutwa na hatia ya kumpa ujauzito mtoto wake wa kufikia ambaye ni mwanafunzi.

Agosti 25, mwalimu wa Shule ya Sekondari Nanga, Keby Aaron (32), alifikishwa mahakamani kwa tuhuma za kumbaka mwanafunzi wa kidato cha tatu (jina lilihifadhiwa) mwenye umri wa miaka 17.

Siku hiyo hiyo, mwalimu wa Shule ya Msingi Chalantai, Tabita Mwanyanjea (29) mkazi wa Nkasi mkoani Rukwa alidaiwa kuuawa na mumewe kwa kuchomwa na kisu shingoni, kwa kilichodaiwa kuwa ni wivu wa mapenzi.

Agosti 27, Jeshi la Polisi mkoani Kagera, lilimshikilia Derick Dambuve (26), mkazi wa wilayani Ngara, kwa tuhuma za kumuua mama Helda Amoni (28) na watoto wake wawili, baada ya kukataliwa kimapenzi na mama huyo.

Agosti 28, Askari wa Jeshi la Akiba, Said Katimbe (49), mkazi wa Tunduru mkoani Ruvuma, aliuawa kwa kuchomwa mkuki kifuani.

Septemba 6, Mahakama ya Wilaya ya Lindi, ilimuhukumu Athumani Mussa mkazi wa Milola, kifungo cha miaka 30 jela kwa hatia ya kumbaka mtoto wa mwajiri wake.

Aidha, mahakama ilimuhukumu Hamza Ahmadi (25) kutumikia kifungo cha miaka 30 jela, baada ya kukutwa na hatia ya kumbaka mwanamke mwenye umri wa miaka 55.

Pia mkoani Kigoma, Mwalimu wa Shule ya Sekondari Kihenya, aliuawa kwa kupigwa risasi na watu wasiojulikana akiwa nyumbani kwake ikidaiwa ni kulipa kisasi.

Septemba 11, Mahakama ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Singida ilimhukumu Hussein Azizi (34) kutumikia kifungo cha maisha jela baada ya kikiri kosa la kumlawiti mtoto mwenye umri wa miaka minne.

**ITAENDELEA KESHO**


## Lawyers' Environmental Action Team (LEAT)

### Publication of Bi Annual Income and Expenditure.

Lawyers' Environmental Action Team is, local Non-Governmental Organization which was found in 1994 and is registered under the NGOs Act of 2002 with (Certificate of Compliance No. 1985).

**Vision**: Tanzania with sustainable and well-managed environment and natural resources for current and future generations.
**Mission**: To contribute towards good governance in the use and sustainable management of the environment and natural resources through public interest litigation, advocacy, strategic research, capacity building, and networking.

In accordance with Non-Governmental Organization (Amendment) Regulation, 2018, the Lawyers Environmental Action Team (LEAT) is pleased to publish the amount of funds received and expended from January 2021 to June 2021.

**Bi-Annual Income and Expenditure for the period from January 2021 to June 2021**

**Income:**

| | |
|---|---|
| Receipt from Donors | 721,577,779.75 |
| Bank Interest | 149,012.70 |
| **Total Income** | 721,726,792.45 |

**Expenditure on:**

| | |
|---|---|
| Legally empower Urbanites living in Dar es Salaam to access and enforce a right to live in clean environment | 120,700,309.06 |
| Examining the Extractive Legal regime in Tanzania | 13,816,515.35 |
| Usimamizi Endelevu wa Maliasili in Tanzania | 544,481,678.08 |
| Collective Action for Rights Realization in the Extractive Industry | 17,346,608.44 |
| Human & Admininistration Resources Activities | 25,381,681.52 |
| **Total Expenditure** | **721,726,792.45** |

In sum, LEAT received grants from the following donors: Legal Services Facility (LSF), Open Society Initiative for Eastern Africa (OSIEA), United States Agency for International Development (USAID-Tanzania) and VSO-Tanzania.

Lawyers' Environmental Action Team (LEAT),
Mazingra Street, MikocheniB, House No 8,
P.O. Box 12605, Dar es Salaam;
Email: info @leat.or.tz.

216373902


# Kampuni, mashirika zatakiwa kuwekeza teknolojia

**Na Joseph Mwendapole**

SERIKALI imetoa wito kwa mashirika na kampuni binafsi za afya nchini kuwekeza katika miundombinu na teknolojia ili kuharakisha utekelezaji wa mikakati ya kitaifa inayolenga kufikisha huduma za afya kwa mamilioni ya Watanzania wahitaji, mpaka vijijini.

Hayo yalisemwa jana na Naibu Waziri wa Afya, Dk. Godwin Mollel, wakati wa uzinduzi wa mashine ya MRI katika Hospitali ya TMJ kwenye hotuba iliyosomwa na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Jayaka Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi.

Naibu Waziri alisema uwekezaji wa sekta binafsi katika teknolojia za kisasa za afya ni jambo muhimu litalosaidia serikali kukabiliana na matatizo mengi ya afya yanayowakabili Watanzania.

"Kuna Watanzania wengi wanaokabiliwa na matatizo mbalimbali ya afya, hasa maeneo ya pembezoni. Vituo vya afya na taasisi za serikali, haziwezi kuwafikia watu wote hawa," alisema.

"Leo hii tunashuhudia TMJ wakizindua mashine ya MRI, ya kisasa, inayotumia teknolojia ya kiwango cha juu... nawahimiza wadau wengine wa afya kuwekeza katika teknolojia kama hizi ili kuwasaidia Watanzania, ambao wengi wao ni maskini," alisema Mollel wakati wa hafla ya uzinduzi wa MRI uliofanya katika kliniki maalamu ya TMJ (Super Specialized PolyClinic) iliyopo Wilaya ya Temeke-Dar es Salaam.

Alisema serikali itaendelea kutoa ushirikiano mkubwa kwa mashirika, kampuni na wadau wengine wa afya (kutoka ndani na nje) katika kuhakikisha Watanzania wanapata huduma bora za afya na zenye viwango.

Kwa upande wake, Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya TM, Dk. Tayabali Jafferji, alisema uzinduzi wa mashine ya kisasa ya upamaji wa magonjwa 'MRI' ni sehemu ya mkakati wake wa muda mrefu wa kusaidia juhudi za Serikali ya Awamu ya Sita zinazolenga kuboresha utoaji wa huduma za afya nchini.

# Shahidi aeleza alivyopigwa, kuteswa na Sabaya

**Na Allan Isack,** ARUSHA



Aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya, akipanda gari kurudishwa mahabusu ya Gereza kuu la Kisongo Arusha, baada ya kuahirishwa kusikilizwa kwa kesi inayowakabili katika Mahakama ya Hakimu Mkazi Arusha. **PICHA: ALLAN ISACK.**

SHAHIDI wa nne upande wa Jamhuri, Hajirini Saad (32), jana amedai mahakamani kupigwa, kuteswa, kuwekwa chini ya ulinzi pamoja na kulazwa kifudifudi na aliyekuwa Mkuu wa Wilaya ya Hai mkoani Kilimanjaro, Lengai Ole Sabaya (34), wakati akitenda uhalifu katika duka la Mohamed Saa lililoko eneo la Soko Kuu jijini Arusha.

Wakili Mwandamizi wa Serikali, Abdalah Chavula, ndiye aliyekuwa akimuhoji shahidi huyo ambaye alitaka kujua shahidi anajishughulisha na nini na Februari 9, mwaka huu, alikuwa wapi. Shahidi alisema ni mfanyabiashara wa mapazia, mashuka, vyandarua na mazuria na siku hiyo alikuwa nyumbani kwake na kuipigiwa simu na kaka Mohamed Saad, akimwambia kuna wateja dukani kwake wanataka kununua mapazia kwa bei ya jumla.

Pia, aliiambia mahakama kuwa alimpigia simu tena kumjulisha simu hiyo ilikuwa ya vitisho na watu waliopiga ni maofisa kutoka Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), na kumuuliza kama ataweza kwenda dukani kuwaangalia watu hao na alimjibu atakwenda kwa kuwa nyumbani kwake ni karibu na dukani hapo.

Alisema alimuaga mke wake na mtoto, lakini mtoto wake aling'ang'ania aende naye na alimchukua kwenda naye dukani.

Shahidi huyo alisema alipofika alikuta mlango umerudishiwa na aliufungua na kuingia ndani dukani.

Alidai alipoingia tu akavutiwa ndani yeye na mtoto wake kwa kuwa kulikuwa na watu ndani dukani.

Shahidi alidai watu walikuwa wengi dukani wengine hakuwafahamu, lakini alipotazama vizuri alimuona Mkuu wa Wilaya ya Hai Lenga Ole Sabaya akiwa na watu wengine.

**Swali:** Shahidi kabda ya siku hiyo, kwenda dukani ulishawahi kwenda kwenye duka hilo mara ngapi?

**Jibu:** Nimekwenda mara nyingi kwa kuwa ni dukani kwa kaka yangu na wakati mwingine amekuwa akiniachia duka kumsaidia kuuza.

**Swali:** Kwa unavyolijua duka hilo, kwa urefu lina mita ngapi na upana wake?

**Jibu:** Duka hilo lina urefu wa zaidi ya mita 10 na upana mita kama nne.

**Swali:** Je, ulipofika ndani ya duka uliona nini huko?

**Jibu:** Nilimuona DC wa Hai, Ole Sabaya, akiwa na watu wengine huko dukani.

**Swali:** Pale uliposimama wewe na alipokuwa Sabaya kulikuwa na umbali gani?

**Jibu:** Kulikuwa na umbali kama wa mita mbili na nusu.

Shahidi alidai alipomuona Sabaya, ulimuita Mheshimiwa Ole Sabaya, na yeye (Sabaya) alimuuliza wewe ndio Mohamed Hajirini? Akamjibu hapana sio yeye.

Alidai kuwa Sabaya alimuuliza amefuata nini hapo na akamjibu kuwa kaka yake alimwambia aende kuangalia kama kuna shida imetokea dukani kwa kuwa kuna watu wapo hapo.

Alidai kuwa mmoja wa watu waliokuwapo dukani alimshika mtoto wake na yeye aliwaambia wamuachie mtoto aondoke kwa kuwa hana kosa na kwamba kama wasingefanya hivyo kingenuka kwa kuwa angepigana nao kwa sababu sio kwamba hafahamu sheria.

Shahidi huyo alisema Sabaya aliagiza wamfungulie mtoto wake (mwenye umri miaka minane), aondoke kwenda nyumbani.

Alidai geti liligongwa kwa nje watu waliokuwa nje walifungua na mtoto akaruhusiwa kuondoka na Sabaya aliagiza apekuliwe.

Alipopekuliwa alidai walichukuwa simu yake, ufunguo wa pikipiki, vitambulisho na leseni ya udereva.

Alidai baadaye walichukua simu na funguo za pikipiki na kumrudishia leseni na vitambulisho vyake.

Wakili alipomuuliza shahidi kama alishawahi kumuona wapi huyo mtu anayemtaja kwa kumwita Sabaya, alisema hajawahi kuonana naye bali alimuona kwenye vyombo vya habari.

**Swali:** Wale watu waliokuwa dukani wanaouza wakati huo walikuwa wapi?

**Jibu:** Nilipovutiwa ndani nilimuona mtu mmoja mzee amelazwa chini na amelala kwa tumbo.

**Swali:** Je, kuna mwanamke ulisema alikuwa amefungwa pingu dukani ulimfahamu?

**Jibu:** Kwa wakati huo sikumfahamu.

**Swali:** Je, hapo dukani ulishuhudia nini?

**Jibu:** Nimuona Numan Jasini, mjomba wangu akiwa pembeni yangu na amepigishwa magoti.

**Swali:** Hebu endelea kuieleza mahakama nini kiliendelea au kilijiri huko dukani?

**Jibu:** Walimgeuza mtu mmoja ambaye alikuwa kwa tumbo chini ya sakafu ndio nikamtambua kuwa ni mzee Salimu ambaye ni fundi umeme na anatutengenezeaga vitu.

**Swali:** Baada wewe kuwekwa chini ya ulinzi, huyo Sabaya alisemaje?

**Jibu:** Alikuwa akituambia sisi tunabadilisha fedha kigeni (Dola) na aliendelea kutuambia kwamba sisi ni wahujumu uchumi na tumeshirikiana na dada yule kuiba dola 70,000 huko Moshi mkoani Kilimanjaro.

**Swali:** Nini sasa kilifuata baada ya matamshi hayo?

**Jibu:** Walimtisha na kumuamsha huyo dada wakimwambia kwamba alikwenda dukani hapo kubadilisha Dola ambazo walishirikiana kuziiba kule Moshi.

**Swali:** Hebu ieleze mahakama sakata hilo lilivyokuwa likiendelea, ulichukua hatua gani?

**Jibu:** Numan, alikanusha kwa kumwambia Sabaya kuwa hawabadilishi Dola na Sabaya aliagiza dada huyo afunguliwe pingu aliyokuwa amefungwa.

**Swali:** Umesema huko ndani aliingia mtu mwingine ni nani na ulimtambuaje?

**Jibu:** Aliingia Bakari Msangi, Diwani wa Kata ya Sombetini na nilimfahamu kwa kuwa ni mtu ambaye tunasali naye msikiti mmoja.

Alipoingia Bakari alisalimia kwa kusema Mheshimiwa Lengai Ole Sabaya habari yako, lakini hakujibiwa kitu. Alirudia kusalimia kwa mara nyingine, lakini hakujibiwa.

Shahidi alidai kuwa Sabaya alimuuliza Bakari kwani hafahamu cheo chake na yeye ni nani? Alimtaka kumuita kwa jina la DC Lengai Ole Sabaya.

**Swali:** Je, baada ya Sabaya kutikia salamu hiyo nini kilitokea?

**Jibu:** Alimuuliza Bakari yeye ni nani na amekwenda kufanya nini hapo dukani na Bakari alimwambia kuwa yeye ni Diwani wa Sombeni na amepigiwa simu na rafiki yake Ali Saad kuwa Sabaya yupo dukani kwake.

**Swali:** Je, siku hiyo mwonekano wa Sabaya ulikuwaje?

**Jibu:** Alikuwa mweusi, mrefu wa wastani, mnene, alikuwa amevaa kaunda suti ya rangi ya bluu na miwani.

**Swali:** Sasa shahidi huyo mtu unaweza kumtambua kama yupo humu ndani mahakamani hebu nenda ukamshike bega kama umemuona.

**Swali:** Je, Sabaya aliagiza upewe simu yako ili ufanye nini?

**Jibu:** Alinipa simu ili kumpigia simu Mohamed Hajirini ili aende dukani kwa kuwa walikuwa wanamwitaji.

Pia, shahidi alidai Sabaya, alimwambia Msangi amsalimie kwa kumwita Jenerali DC Sabaya, na baada ya kumsalimia kama alivyotaka alimwambia kwa nini anashirikiana na Waarabu.

Alidai wameshirikiana na yule dada kuiba Dola 70,000 na wamekuwa wakimbadilishia kwenye duka hilo na kuwaambia wao ni majambazi na wahujumu uchumi.

Pia alikwenda kuchukua begi la mkononi la yule dada na alifungua na kutoa kati ya Dola 100 au 200.

Shahidi alidai Msangi alimwambia yeye ni Mkuu wa Wilaya ya Hai, na Arusha kuna DC, TRA na vyombo vya dola na akiangalia hapo hawaoni hata mmoja wao.

Alidai Sabaya aliwaagiza walinzi wake kumtoa lockup Msangi kwa kumpiga kipigo kizito. Alipigwa makofi ya masikioni na usoni na kichwani alilia sana kwa sauti kwa kusema Mheshimiwa Sabaya, anampiga kwa kosa gani na waliendelea kumpiga hata alipoanguka chini walimsimamisha tena na kuendelea kumtembezea kipigo.

Kabla ya kupigwa Sabaya aliwaagiza walinzi wake kumsachi Msangi na walimchukulia waleti na simu yake, lakini alirukia kwenye mguu wa Sabaya huku akimwomba msamaha akimweleza kwamba mke na mtoto wake ni wagonjwa.

"Lakini aliagiza walinzi wamtoe na waendelee kumpiga sehemu za usoni na kichwani na Msangi alipiga sana kelele kutokana na kipigo alichopigwa."

"Bakari Msangi alilia kwa kusema Meya wa Manispaa na Moshi (Juma Raibu) mdogo wangu ni rafiki yako.

Shahidi alidai kipigo kilitendeka kwa zaidi ya nusu saa.

Alidai pia Sabaya alikuwa ameshika bastola nyeusi aliyokuwa akipokeza na walinzi wake kuwatishia na walikuwa wamebeba 'radio call' ambayo waliitumia kuwasiliana na watu wengine waliokuwa nje ya duka.

"Siku hiyo nilikuwa nimefunga niliomba maji, lakini walininyima kwa kuwa mimi ni mtu wa ibada nilitabasamu nikiwa nimekaa chini kufikiria kile kilichotokea na mmoja wa walinzi wa Sabaya alisema Mheshimiwa huyu anacheka inaonekana anaona kuwa jambo hili siyo la muhimu," alidai shahidi.

Alisema mtu aliyezungumza maneno hayo alikuwa mnene wa wastani na mrefu wa saizi ya kati, ana rangi ya maji ya kunde.

Shahidi alidai kuchukuliwa na kuingizwa kwenye chumba cha kuhifadhia majora ya vitambaa na Sabaya aliagiza apigwe ili atolewe ngewe.

Pia, alidai kuwaambia walinzi wake waendelee kumpiga kwa kuwa kipigo hakikutosha, pia alimwambia nimwite kwa jina la General More Power, nilitekeleza alichotaka nilimwambia hii ni dunia leo kwangu kesho kwako.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# *Kuzingatia mwongozo mpya corona muhimu*

**SERIKALI** imekuja na mwongozo mpya wa kupambana na virusi vya corona, huku ikipiga marufuku mikusanyiko mikubwa ya kijamii, zikiwamo sherehe, shughuli za kisiasa na kidini isiyo ya lazima.

Katika taarifa yake kwa umma, Katibu Mkuu wa Wizara yenye dhamana na afya za Watanzania, Prof. Abel Makubi, alisema, marufuku hiyo inakuwapo hadi ugonjwa huo utakapodhibitiwa na taarifa kutolewa rasmi.

Serikali inasema inachukua hatua hiyo, kutokana na mwenendo wa ugonjwa huo nchini, na kwamba kamati ya wataalamu imeainisha maeneo mahususi yanayohitajika kutiliwa mkazo kupitia afua za kupunguza msongamano katika jamii, ili kukata mnyororo wa maambukizi katika ngazi ya kaya na jamii.

Kwa mujibu wa Prof. Makubi, mwongozo huo utawawezesha wananchi kufanya shughuli zao za kiuchumi na kijamii na kubadili tabia zao huku wakizingatia mbinu za kujikinga na corona, kwa kupata elimu ya kutosha na kujiwekea utaratibu wa kudhibiti ugonjwa kutokusambaa kwenye jamii.

Mwongozo huo unalenga maeneo yenye mikusanyiko ya watu, hasa ya huduma za kijamii, kibiashara, kiuchumi, kiofisi, ambayo ni mojawapo ya vyanzo vya kusambaa kwa maambukizi katika jamii.

Kwingine ni katika vituo vya mabasi, ambapo mwongozo unaelekeza uongozi wa vituo hivyo, kusimamia uwapo wa vifaa vya kunawia maji tiririka na kuhakikisha abiria wote wananawa mikono.

Wamiliki wa vyombo vya usafiri nao wanatakiwa kuweka vitakasa mikono katika vyombo hivyo na kusimamia uvaaji barakoa, huku wale wanaohitaji kufanyika shughuli za mikusanyiko wakitakiwa kuomba vibali maalum.

Sisi tunaunga mkono juhudi hizo za serikali, na tunaushauri umma wa Watanzania kuuzingatia, kwani uzoefu unaonyesha kuwa tangu kutangazwa kwa wimbi la tatu la corona, baadhi ya watu hawajachukua tahadhari zozote.

Kuanzia katika vyombo vya usafiri na hasa daladala, abiria wanajazana kupita kiasi, hawavai barakoa, kwenye vituo hakuna maji wala vitakasa mikono, na hata baadhi ya kumbi za starehe hali ni ile ile.

Tunadhani hali hiyo ya baadhi ya watu kutokuwa makini na ugonjwa huo, aidha inatokana na ukosefu wa elimu ya kutosha kuhusu madhara ya corona, au wanafanya makusudi.

Lakini pamoja na yote hayo, njia ambayo tunaamini inaweza kusaidia, ni kuendelea kutolewa kwa elimu ili jamii ibadilike, kwani kumekuwapo na elimu nyingi ambazo hutolewa mitaani na watu wasio wataalamu wa afya.


Kwa hali kama hiyo, wakati mwongozo ukiwapo, tunadhani ni wakati mwafaka wa kutolewa kwa elimu hiyo kwa wingi, ili kuwabadilisha Watanzania ambao bado hawaamini kuwapo kwa ugonjwa huo nchini ili wachukue tahadhari.

Lakini tungeshauri kuongezwa kwa magari ya abiria hasa maeneo ya mijini kama Dar es Salaam ambako abiria wamekuwa wakijazana katika daladala kupita kiasi kutokana na uhaba wa usafiri.

Kutokana na mwongozo kuelekeza vyombo vya ulinzi na usalama kuhakikisha mabasi ya usafiri wa umma yanapakia abiria kulingana na idadi ya viti pasipo kusimama, tunashauri kuongezwa kwa mabasi ya abiria.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED

**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com



## Muungwana Lazima Nilonge



Na Christina Mwakangale

# *Sare makonda, madereva zilivyo adhabu kwa abiria*

**MAKONDAKTA** na madereva wa mabasi ya mijini na kwenye majiji zikiwamo daladala jijini Dar es Salaam, wanakera linapokuja suala la kuvaa sare ambalo hawalizingatii licha ya kwamba ni utaratibu.

Makondakta pamoja madereva ni kama vile hawataki kuvaa sare hizo, wakati wengine wanashangaza kwa uchafu, uchakavu na kupauka kwa nguo hizo.

Mathalani, yuko anayevaa shati lenye mkono mmoja uliokatwa, wakati mwingine umeraruka, hakuna vifungo, vazi ni kubwa kuliko kipimo chake, suruali hazina zipu na muda mwingine zinawavuka, lakini cha kushangaza ndani wamevaa bukta au boksa ambazo zinaonekana.

Wakati mwingine ni kawaida sare hizo zinalalamikiwa kuwa zinanuka na miguuni madereva na makonda wanavaa makubazi au raba chafu zinazotoa harufu pia. Vijana hao hawachani nywele, lakini wana lugha mbaya na kejeli kwa abiria.

Kwa ujumla kuchezea sare kunaelekea kuwa sugu hata mamlaka za usimamizi katika hili zimepungua kasi ya kuwakemea, ikiwamo trafiki ambao kazi kubwa imekuwa ni kuwapiga faini huku Mamlaka ya Udhibiti wa Usafiri wa Ardhini (LATRA), zikikaa kimya kwenye usafi wa mwili.

Usafiri kafiri! Walijisemea wahenga. Usafiri huu unaonekana ni kama bora liende, daladala ni chafu, hakuna vyombo vya kuwekea taka, hata kama kipo wakati mwingine ni balaa kwa abiria vinaning'inia juu ya vichwa vyao na vimejaa taka ambazo zinanuka.

Sare hizi inavyooneka makondakta na madereva wanazo moja au wanachangia pengine ni kwa sababu zinauzwa ghali huko zinakopatikana.

Sare zinavaliwa zikiwa chafu kutoka Jumatatu hadi Jumatatu, sasa 24, siku 365 za mwaka hakuna mabadiliko yoyote.

Sare hizi ni kero kwa abiria, hasa pale kondakta anapobanana nao kwenda mbele na nyuma kukusanya nauli hasa wakiwa wamebanana kupindukia bila kujali kuwa kuna corona .

Jamii haipaswi kulikalia kimya kwani hii ni huduma kama zilivyo nyingine uvaaji wa sare hizi upo kulingana na sheria, kanuni na taratibu za usafirishaji katika usafiri wa umma.

Ushuhuda ni kwamba usafiri wa mabasi yaendayo mikoa tofauti na nchi jirani wanajitahidi kuvaa sare safi na unadhifu humvutia mteja na uvaaji wa sare haujaanzia au haupo tu kwa makondakta na madereva.

Maeneo mengi ikiwamo sare katika sekta, idara, taasisi na ngazi tofauti kwa lengo la kuongeza weledi kwenye kutoa huduma, kuweka utambulisho wa wahusika na kuongeza unadhifu.

Sare licha ya kuvaliwa na watu wengi kama polisi, wanajeshi, wauguzi, manahodha ya meli, rubani wa ndege usafi wa mavazi hayo ni muhimu ili kuhudumia wateja na kuepusha usumbufu.

Pamoja na kuzungumzia masuala ya kuweka nauli na kuainisha viwango vinavyotakiwa kutozwa kwa abiria, mamlaka wadhibiti wanawajibika pia kushughulikia usafi wa makondakta na uvaaji wa sare kikamilifu.

Hakika wananchi wanakerwa na uvaaji wa makondakta na madereva ambao huchangia pia uendeshaji wa kivurumai, matusi na lugha mbaya kwa wateja hasa linapokuja suala la kuwasindilia abiria kwenye magari bila kujali afya na usalama wao na mizigo waliyo nayo.

Heshima ya kazi ya mtu huanzia na mhusika mwenyewe ndipo wengine wataiheshimu kazi yake, mtindo wa kuzivaa nguo ambazo hazina unadhifu, shati kubwa, suruali inayoning'inia miguuni na zinazofungwa kwa kamba za mkonge achilia mbali uchafu wa mwili kunawafanya watu wasiwathamini wahusika.

Tatizo hilo la kukosa sara nalo liko kwa madereva wa pikipiki. Waendesha boda boda nao ni wachafu na pengine ni wakati wa mamlaka zinazohusika kuona umuhimu wa kuwahimiza kubadilika.

HABARI KITAIFA

## DC aagiza mfamasia kituo afya asimamishwe

**Na Shaban Njia,** KAHAMA

MKUU wa Wilaya ya Kahama mkoani Shinyanga, Festo Liswaga, amemwagiza Mganga Mkuu wa Halmashauri ya Ushetu, Dk. Nikodemas Maganga, kumsimamisha kazi mfamasia wa Kituo cha Afya Bulungwa, Jastine Mtimba, kwa tuhuma za kuwatoza Sh. 5,000 za matibabu kinamama wenye watoto chini ya miaka mitano.

Kiswaga alitoa maagizo hayo baada Jastine kukamatwa na wajumbe wa kamati ya siasa ya Chama Cha Mapinduzi (CCM) iliyotembelea kituo hicho kukagua utekelezaji wa ilani ya uchaguzi ya chama hicho ya mwaka 2020- 2025.

Alisema serikali haitawavumilia watumishi wa umma watakaobainika kukiuka maadili na miongozo ya kazi zao, kwa kujihusisha na vitendo vya rushwa katika maeneo ya kutolea huduma, kitendo hicho ni kinyume cha maelekezo ya Wizara ya Afya, Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto.

Aliongeza kuwa serikali imeagiza watoto chini ya miaka mitano na wazee wenye miaka 60 wanapate huduma za afya bure na hawapaswi kutozwa gharama zozote, na kwamba anashangaa mfamasia anavyowatoza shilingi 5,000 kinamama wenye watoto chini ya miaka mitano. Kiswaga aliwataka watumishi wa Halmashauri za Ushetu, Msalala na Manispaa ya Kahama kuwa wazalendo na kujiepusha na vitendo vya rushwa, kwani vinasababisha wananchi hasa wanyonge kuichukia serikali bila sababu za msingi.

Kwa upande, Dk. Maganga alisema, agizo la kumsimamisha kazi mfamasia huyo amelipokea na atalifanyia kazi kulingana na taratibu za kiutumishi na atampelekea mrejesho Mkuu wa Wilaya kuhusu maamuzi yaliyofanyika.

Kaimu Mwenyekiti wa CCM Wilaya ya Kahama, Emmanuel Mbamange alisema, kituo hicho kimekuwa na malalamiko mengi ya wagonjwa dhidi ya watoa huduma, na kwamba baadhi ya watumishi wa afya wamekuwa wakiwauzia wagonjwa dawa zao binafisi kituoni.

Naye Mkazi wa Kata ya Bulungwa, Elizabeth Marando, aliyefika kituoni kupata matibabu, alisema, katika kituo hicho watoto chini ya miaka mitano wamekuwa wakitozwa fedha za kumwona daktari na matibabu, lakini hawapewi risiti za malipo.

Alisema mtu akienda na mtoto chini ya miaka mitano bila shilingi 10,000 hapati matibabu, hivyo anatakiwa kutoa shilingi 5,000 za kumwona daktari na shilingi 5,000 nyingine kwa ajili ya dawa, hali ambayo imewafanya baadhi yao kianza kwenda kwa waganga wa jadi kupata huduma.

## SAHIHISHO

Katika chapisho la gazeti hili toleo la jana Julai 26, 2021 ukurasa wa saba linalohusu **CHAMA CHA WAFANYAKAZI WA TAASISI ZA ELIMU YA JUU TANZANIA** lenye kichwa cha habari **TANGAZO NAFASI YA KAZI**, kipengele sifa za mwombaji aya ya tatu, kuna maneno kwa bahati mbaya hayakuonekana. Maneno hayo yanapaswa kusomeka:(iii) Awe na uzoefu wa kazi katika ngazi ya menejimenti ya vyama vya wafanyakazi kwa muda usiopungua miaka mitano (5).

***Samahani kwa usumbufu uliojitokeza- Mhariri.***

# Mghwira azikwa, aenziwa kwa kujengewa barabara

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), Ummy Mwalimu, ameongoza mamia ya wananchi wa Mkoa wa Arusha katika mazishi ya aliyekuwa Mkuu wa Mkoa wa Kilimanjaro, Dk. Anna Mghwira.

Akitoa salamu za pole kwa niaba ya Rais Samia Suluhu Hassan, Ummy alisema Dk. Mghwira alikuwa ni mwanamke shupavu, mchapakazi aliyefanya kazi kwa bidii bila kulalamika hata pale alipokutana na changamoto.

Alisema katika kumuenzi Dk. Mghwira alimwagiza Meneja wa Wakala wa Barabara Vijijini na Mijini (TARURA) Mkoa wa Arusha kujenga barabara ya lami kutoka barabara kuu ya Bay pass hadi nyumbani, ipewe jina la "Anna Mghwira".

Alisema Dk. Mghwira ameacha alama katika uongozi na alithubutu hata kugombea nafasi kubwa ya uongozi wa juu nchini ya urais mwaka 2015.

Alisema taifa limepoteza kiongozi mwenye utumishi uliotukuka. Alisema marehemu Dk. Mghwira anapaswa kuigwa kwa uongozi wake ambao alitumikia nafasi mbalimbali za kitaifa na kimataifa na aliacha alama.

Baada ya kumalizia salamu hizo aliwakilisha rambirambi ya Rais Samia Suluhu Hassan kwa familia ya marehemu.

Mkuu wa Mkoa Kilimanjaro, Dk. Stephen Kigaigai, alisema marehemu alikuwa zaidi ya kiongozi kwake kwani hakusita kumpa mbinu alizotumika kuongeza.

"Hata baada ya kustaafu nilipokuja nampigia simu kuomba ushauri hakusita kunielekeza, kweli kwangu huyu mama alikuwa mwalimu," alisema.

Akitoa salamu za Mkuu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Askofu Dk. Fredrick Shoo, Katibu Mkuu wa Dayosisi ya Meru Lazaro Urioh, aliwataka wananchi wa waumini wa kanisa hilo kuendelea kuchukua tahadhari zote muhimu za kukabiliana na ugonjwa wa corona wakati wote.

"Wakati serikali inaendelea kuchukua jitihada za kukabiliana na ugonjwa huu ni wajibu wetu sisi waumini kuhimizana kufuata maelekezo ya serikali na kama kanisa tunahimiza umuhimu wa kutumia chanjo za corona zilizoletwa nchini kwa kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya."

Askofu wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Tanzania Dayosisi ya Meru, Dk. Elias Kitoi, alisema marehemu bado alikuwa na dhamira ya kuendelea kuwatumikia Watanzania.

Awali mtoto wa mwisho wa marehemu Elisha Mghwira, alisema marehemu alianza kuugua homa kali ya mapafu Julai 11, mwaka huu na kulazwa katika Hospitali ya Nkaoaranga iliyomililikiwa na Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT) Dayosisi ya Meru, ambapo hakupata nafuu na kuhamishiwa Hospitali ya Rufani ya Mt Meru mkoani Arusha, ambapo alifariki Julai 22, mwaka huu.




Mkurugenzi Mkuu wa Hospitali ya TMJ, Dk. Tayabali Jafferji, akizungumza wakati wa uzinduzi wa mashine ya kisasa ya MRI katika Wilaya ya Temeke, iliyoko Kliniki Maalamu ya TMJ (Super Specialized PolyClinic). Wapili kulia ni Ofisa Mtendaji wa TMJ, Parul Chhaya, Mkuu wa Wilaya ya Temeke, Jokate Mwegelo, na Mkurugenzi Mtendaji wa Taasisi ya Moyo ya Kikwete (JKCI), Prof. Mohamed Janabi. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Aliyehukumiwa maisha jela kisa kubaka kesi kusikilizwa upya

**Na Kulwa Mzee**

MAHAKAMA Kuu Masijala ya Bukoba imemfutia adhabu ya kifungo cha maisha jela Ayubu John kwa kosa la kubaka, na kuamuru kesi ianze upya kwa sababu alisomewa mashtaka kwa lugha asiyoielewa akakili kosa na kutiwa hatiani.

Uamuzi huo ulitolewa mbele ya Jaji Emmanuel Ngigwana baada ya kusikiliza rufani iliyokatwa na Ayubu ikiwa na sababu tano akiomba mahakama hiyo imfutie adhabu aliyopewa. Mrufani alitiwa hatiani na Mahakama ya Wilaya ya Ngara Oktoba 13, mwaka jana, Oktoba 11 mwaka jana alishtakiwa kwa kubaka, aliddaiwa kumbaka mtoto wa miaka nane, tukio hilo lilitokea maeneo ya Lukole Hamnet, kijiji cha Kumnazi, Ngara.

Mrufani alijiwakilisha mwenyewe, huku Jamhuri ikiwakilishwa na Wakili wa Serikali, Juma Mahona.

Katika hoja za rufani, mrufani anaomba Mahakama imfutie kutiwa hatiani na adhabu ya kifungo cha maisha jela.

Anadai mahakama ilikosea kwani alikili kosa katika mashtaka yaliyosomwa kwa lugha ambayo hakuielewa.

Akijibu Wakili Juma alidai mshtakiwa alisomewa mashtaka kwa lugha anayoelewa hivyo aliomba rufani itupwe kwani haina msingi.

Jaji Ngigwana katika uamuzi wake alisema mahakama ya chini ilikuwa na jukumu la kumfafanulia mshtakiwa mashtaka yanayomkabili na adhabu kuhusiana na mashtaka hayo.

Alisema mahakama ilitakiwa kufahamu kwamba mshtakiwa kaelewa makosa anayoshtakiwa nayo ama la.

"Hakuna mahali ambapo mahakama ilifafanua kwa mrufani kuhusu mashtaka yake na adhabu, kumbukumbu hazioneshi lugha gani ilitumika katika kusoma mashtaka kama ni Kingereza au Kiswahili.

"Hakuna kumbukumbu inayoonyesha kama Mahakama ilimuuliza mrufani asomewe mashtaka kwa lugha ipi anayoielewa na kwamba hati ya mashtaka ilitakiwa kusomwa kwa lugha inayoeleweka kwa mshtakiwa," alisema.

Alisema kutokana na mazingira hayo ni wazi kwamba mashtaka yalisomwa kwa lugha ambayo mrufani hakuelewa. Mahakama iliamuru adhabu ya kifungo cha maisha jela ifutwe, kutiwa hatiani kufutwe na kesi ianze upya mbele ya Hakimu mwingine.

Mrufani alitakiwa kuendelea kuwa rumande hadi kesi itakapoanza upya, rufani iko wazi kwa upande utakaopingana na uamuzi huo.

# ‘Wastaafu watarajiwa jihadharini na matapeli’

**Na Richard Makore,**
MWANZA

WASTAAFU watarajiwa ambao ni wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii kwa Watumisihi wa Umma (PSSF), wametakiwa kuwa makini dhidi ya matapeli wanaosubiri kuwapora mafao yao baada ya kustaafu.

Tahadhari hiyo ilitolewa jana jijini hapa na Mkuu wa Mkoa wa Mwanza, Robert Gabriel, alipofungua semina ya siku mbili ya watumishi hao wanaotarajia kustaafu.

Gabriel alisema wakati watumishi hao wakijiandaa kustaafu kuna matapeli wengi wakiwamo ndugu na marafiki wanaofanya vikao kuhakikisha wanapora mafao yao.

Alisema fedha za kustaafu zinatakiwa kulindwa na Mungu pamoja na mbinu zingine za kibinadamu kwa kuwa wabaya ni wengi kuliko wema.

Aliwataka watumishi hao kumwomba Mungu kwa kuwa fedha za kupata kwa mara moja zinambadilisha mtu pamoja na mtindo wake wa maisha aliyozoea kuishi.

Aliongeza kuwa wastaafu wengi baada ya kupata mafao yao hawataki ushauri wowote wa mtu, lakini fedha zinapoisha huwa wanakuwa wapole kama watu waliookoka.

Aliwataka watumishi hao kuendelea kufanya vitu ambavyo wana uzoefu navyo ikiwamo biashara, badala ya kuanzisha shughuli ambazo hawazifahamu na wala hawajawahi kuzifanya.

“Fedha za mafao zina vishawishi vingi utasikia mstaafu anapewe uenyekiti wa msiba, sherehe, kuteuliwa kuwa baba ama mama walezi wa maharusi na pesa zikiisha vyeo vyote anaondolewa,” alisema Gabriel.

Pia aliwataka watumishi ambao wanaokaribia kustaafu kuacha kutoa rushwa ya aina yoyote wakati wakifuatilia mafao yao.

Aliongeza kuwa mtumishi yeyote akiombwa rushwa asisite kutoa taarifa kwa vyombo vinavyohusika ili aliyemuomba aweze kushughulikiwa kwa mujibu wa sheria.

Kwa upande wake, Kaimu Mkurugenzi wa PSSF, Beatrice Lupi, akizungumza katika semina hiyo, alisema mfuko huo unatoa mafao kwa mujibu wa sheria ndani ya siku 60 endapo mstaafu atakamilisha vielelezo vyote muhimu.

Alisema kinachochelewesha wastaafu kulipwa mafao yao kwa wakati ni pamoja mwajiri (serikali) kuchelewa kuwasilisha nyaraka muhimu za mtumishi kwenye mfuko wao.

Beatrice aliwataka wastaafu hao kuheshimu mafao watakayolipwa ili yaweze kuwasaidia katika maisha yao ya uzee baada ya kustaafu.

Aliwataka kujihadhari na matapeli wa aina mbalimbali wakiwamo wanaotaka kuwauzia magari mabovu, kuwauzia nyumba kwa bei kubwa pamoja na kuwashawishi waingie katika biashara wasizozijua.

Jumla ya watumishi 110 mkoani Mwanza walipewa semina na PSSF iliyolenga kuwajengea uwezo, kujiamini pamoja na kufahamu kitu gani wanaweza kuzifanyia fedha hizo baada ya kustaafu.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akizungumza na viongozi, wateja wa Benki ya Exim aliposhiriki hafla ya chakula cha jioni kwa ajili ya wateja jijini Dodoma. Wanaomsikiliza ni Mkuu wa Huduma ya Rejareja, Andrew Lyimo (katikati) na Mkurugenzi wa Bodi ya benki hiyo, Irene Mlola. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Watoa huduma wabainisha athari za tozo miamala simu

**Na Christina Mwakangale**

CHAMA cha Waendesha Huduma ya Simu za Mkononi Tanzania (TAMNOA), kimeelezea athari zilizotokana na tozo katika miamala kupungua.

Kikisema wateja zaidi ya milioni moja, hususani walioko vijijini walisitisha huduma na miamala kupungua kwa asilimia 45.

Licha ya athari hizo zilizotajwa na TAMNOA, kimepongeza hatua ya serikali, kuangalia upya tozo za miamala kwenye simu, hatua hiyo itaongeza chachu ya uwekezaji wa ndani katika sekta hiyo.

Mwenyekiti wa TAMNOA, Hisham Hendi, ambaye ni Ofisa Mtendaji Mkuu wa Vodacom, alisema jana jijini Dar es Salaam kwamba kampuni za simu zinaipongeza serikali kitendo cha kufikiria upya tozo za miamala ya simu.

Hendi alisema Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021/22, iliyopitishwa bungeni ni chanzo cha namna mpya ya utozaji kodi katika kila muamala unaofanywa na mteja kwa njia ya simu za mkononi.

Alisema watoa huduma za simu pamoja na wateja zaidi ya milioni moja, hususani walioko vijijini walisitisha kutumia huduma za miamala ya simu, kutokana na ongezeko la makato, ambayo aliyataja kama tishio kwenye uhai wa biashara ya simu nchini.

“Katika siku chache zilizopita tangu Sheria ya Fedha ilipoanza kutekelezwa Julai 15, mwaka huu, miamala ya wateja ilipungua kwa asilimia 45, jambo ambalo limeathiri mapato ya kampuni za simu, hivyo kupunguza kodi kwa serikali,” alisema Hendi.

“Tunaishukuru serikali kwa kuona umuhimu na tunampongeza Rais Samia Suluhu Hassan na serikali yake kwa kusikiliza kilio cha wananchi.”

Hendi alisema ana imani na matokeo na mapendekezo ambayo yatakayotolewa na kikosi kilichoundwa na waziri mkuu, huku akisisitiza kuwa kampuni za simu zitakuwa na uwezo mkubwa kibiashara nchini.

Aliongeza kuwa Tanzania hivi sasa inajivunia ukuaji wa uchumi barani Afrika kutokana na uwekezaji mkubwa wa kampuni za simu. Awali baada ya malalamiko kuhusu tozo kwenye miamala, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, alifanya kikao na mawaziri pamoja na wadau wa sekta ya mawasiliano, kutatua tatizo hilo na kikao kutoa mapendekezo ya kutafuta ufumbuzi.

Waziri Mkuu aliunda kikosi kufanya kazi hiyo, ambacho hivi karibuni kitakaa na kampuni za simu na Benki Kuu (BoT), kuangalia masuala yahusuyo, kodi ili kuyatafutia ufumbuzi.

Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Emmanuel Tutuba, alisema kikosi hicho kinajumuisha wataalamu kutoka BoT, Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA), Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Wizara ya Mawasiliano na Teknolojia ya Habari.

Takwimu zilizotolewa hivi karibuni na Taasisi ya Masuala ya Mawasiliano (GSMA), huduma nafuu za mawasiliano popote duniani, uwezekano ni wa kuboresha sekta mbalimbali zinazotegemea huduma ya sekta hiyo, hasa kilimo na afya.

Bunge lilipitisha Sheria ya Fedha ya Mwaka 2021/22, ambayo ni mpya inayotoza kodi ya miamala ya simu ambayo iliyosababisha malalamiko.

Aidha, Waziri wa Fedha na Mipango, Dk. Mwigulu Nchema, alisema ma Rais Samia amesikiliza kilio cha wananchi na kutoa maelekezo ya namna ya kushughulikia suala hilo.

## Mtaka ataka uwezeshaji makandarasi wa ndani

**Na Mwandishi Wetu,**
DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, ametoa wito kwa Benki ya Exim Tanzania kuangalia namna ya kuwawezesha makandarasi wa ndani ya nchi ili waweze kutekeleza miradi mikubwa ndani na nje ya nchi.

Mtaka alitoa wito huo mwishoni mwa wiki aliposhiriki kwenye hafla ya chakula cha jioni iliyoandaliwa na Benki ya Exim, kwa ajili ya wateja wake wa jijini Dodoma, ambapo alitolea mfano wa Benki ya Exim China, ambayo imekuwa ikiwawezesha makandarasi kutoka nchini humo kutekeleza miradi mikubwa nje ya nchi ikiwamo Tanzania.

“Nimefurahishwa na ufunguzi wa tawi jipya la Benki ya Exim jijini Dodoma, hivyo basi pamoja na kuongeza mtandao na huduma kwa wateja wenu, nashauri ni vema zaidi pia muangalie namna ya kuwasaidia makandarasi wetu wa ndani ili waweze kutekeleza miradi mikubwa ndani na nje ya nchi ikiwamo kwenye mataifa ambayo i benki ina matawi yake ikiwamo Comoro, Djibouti, Uganda na Ethiopia,” alisema.

Alisema kwa kuwa kampuni kubwa zinazotekeleza miradi yake nchini zimekuwa zikiwezeshwa kifedha na benki katika mataifa yao, ipo haja pia kwa benki nchini kuiga mfano huo.

Mtaka aliiishauri benki hiyo kuangalia namna ya kusaidia kupunguza tatizo la ajira kwa vijana wanaohitimu vyuo kwa kufadhili miradi inayotokana na mawazo yao kwa kuanzisha mfuko maalumu unaofanana na ule wa uwajibikaji kwa jamii (CSR).

Mkurugenzi wa Bodi ya benki hiyo, Irene Mlola, alisema benki hiyo imepokea ushauri wa Mtaka na kuahidi kuuafanyia kazi, huku akisisitiza uwapo wa tawi la benki hiyo jijini Dodoma ni mwanzo wa kuwasaidia wakazi wa jiji hilo kukuza uchumi wao kwa kuwasogezea huduma za kifedha karibu zaidi katika kuhakikisha kwamba huduma hiyo inawafikia wananchi wote hususani waliopo pembezoni.Alisema benki hiyo pia imekuwa mstari wa mbele kuhakikisha inashiriki kikamilifu kujenga uchumi wa nchi kwa kushirikiana na serikali na zaidi sekta binafsi ili kufanikisha uchumi wa viwanda.

Mkuu wa Huduma za Wateja Wadogo na wa Kati wa benki hiyo, Andrew Lyimo, aliahidi kuwa wamejipanga kutoa huduma zinazoendana na mahitaji yao.

# RC Mkirikiti atoa hadhari ya corona

**Na Gurian Adolf,** SUMBAWANGA

MKUU wa Mkoa wa Rukwa, Joseph Mkirikiti, amewataka wakazi wa mkoa huo kuhakikisha wanafuata maagizo yote yaliyotolewa na Wizara ya Afya katika kujikinga na ugonjwa wa Uviko 19.

Agizo hilo alilitoa jana wakati akizungumza na wakazi wa mkoa huo kupitia kituo kimoja cha redio.

Amesema kuwa wananchi wanapaswa kutekeleza maagizo yaliyotolewa na serikali kupitia Wizara ya Afya kwani awamu hii ya tatu ya ugonjwa huo ni hatari zaidi kwani hali ni mbaya.

Aliwaondoa hofu wakazi wa mkoa huo ambao wamekuwa wakilalamikia kukosekana kwa soko la zao la mahindi kuwa hivi karibuni serikali kupitia Wakala wa Chakula (NFRA) itaanza kununua mahindi, hivyo bei itapanda.

Aliwataka wakulima kuendelea kuzalisha mazao mbalimbali yakiwamo ya chakula kwani serikali inaendelea na mikakati ya kutafuta soko la uhakika la mazao yao.

Pia Mkirikiti aliwataka wananchi kujenga utamaduni wa kuwahoji viongozi wao maendeleo ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kwani kuhoji kunasababisha miradi hiyo itekelezwe kwa kiwango kwa kuwa wananchi watakuwa wakiifuatilia.

Kadhalika, aliwataka wananchi kuitunza miradi iliyotekelezwa na serikali katika maeneo yao kwani ni muhimu waitunze ili idumu na itawafaa kwa muda mrefu.

**Aliwaondoa hofu wakazi wa mkoa huo ambao wamekuwa wakilalamikia kukosekana kwa soko la zao la mahindi kuwa hivi karibuni serikali kupitia Wakala wa Chakula (NFRA) itaanza kununua mahindi, hivyo bei itapanda.**

# Walipwa kifuta jasho mil. 74/- mazao kuliwa na tembo

**Na Sabato Kasika,** LIWALE

JUMLA ya Sh. milioni 74.7 zimelipwa kama kifuta jasho kwa wakulima 279 Kata ya Kibutuka, Wilaya ya Liwale mkoani Lindi, ambao mazao yao yaliharibiwa na tembo hivi karibuni.

Hayo yalisemwa mwishoni mwa wiki na Mkuu wa Wilaya hiyo, Judith Nguli, na kufafanua kuwa wakulima hao ni wa vijiji vya Ngumbu, Mtawatawa, Mkutano na Lilombe.

"Wizara ya Maliasili na Utalii imetoa kifuta jasho hicho kwa wakulima hao, ambao mashamba yao ya mikorosho ilivunjwa matawi, huku ufuta ukikanyagwa na wanyama hao na kufanya uharibifu," alisema Nguli.

Alitaja mazao mengine yaliyoharibiwa na tembo hao kabla ya kuondolewa na askari wa wanyama pori ni yale ya chakula kama mtama, mbaazi na mihogo.

Alisema tembo hao walifanya uharibifu huo Mei mwaka huu, kisha serikali ikafanya tathmini ya uharibifu huo na taratibu nyingine za kisheria zikiwamo za kulipa kifuta jasho ambacho kilimaliziwa kutolewa wiki moja iliyopita.

"Mwishoni mwa mwezi huu, wakulima wataanza kupewa elimu ya jinsi ya kuepuka wanyama hao na pia kuacha mtindo wa kulima mazao kwenye njia za tembo kwa ajili ya usalama wao," alisema.

Ofisa Maliasili wa wilaya huyo, Damas Mumwi, alisema eneo hilo ambalo tembo walivamia ni mapito yao ya miaka mingi, hivyo ni vyema likaachwa wazi ili wanyama hao waendelee kulitumia kama njia.

"Kwa kawaida tumbo huwa hawasahau njia yao na hutoka Rondo kule Mtama, kupitia Nachingwea, Liwale katika pori lililopo karibu na vijiji, wakikuta mashamba wanakula mazao na kuharibu mengine," alisema Mumwi.

Alisema kuwa mapito ya tembo kwa sasa yamevamiwa na wakulima wa ufuta kutoka Newala na Tandahimba mkoani Mtwara na kwamba taratibu za kuhakikisha yanakua wazi, zinaendelea.

Diwani wa Kata ya Kibutuka, Faraji Nyihira, alisema kwa kawaida wakulima wa huko huwa wanajenga vijimba vidogo katika mashamba na kisha uhamia huko, ambayo si salama kwao tembo wanapopita.

"Bahati nzuri walipopita, hakukuwa na mkulima, kwani ingekuwa ni hatari kwa usalama wao, kwani wangeweza kuhatarisha maisha yao na pia kuharibiwa mazao yao," alisema Nyihira.

Diwani huyo alisema, ingawa mamlaka husika imewaondoa tembo hao na kuwapeleka mbuga za Selous, anaomba ufuatiliaji wa karibu uendelee ili kuhakikisha wakazi wa kata yake wanakua salama.




Mkurugenzi Mkuu wa Mfuko wa Fidia kwa Wafanyakazi (WCF), Dk. John Mduma (katikati), akizungumzia kushushwa kwa viwango vya uchangiaji wakati wa mkutano na waandishi wa habari makao makuu ya mfuko jijini Dar es Salaam jana. Waajiri wa sekta binafsi watachangia asilimia sita ya mishahara ya wafanyakazi wao kutoka asilimia moja waliyokuwa wakichangia, wakati sekta ya umma wataendelea kuchangia asilimia tano kama ilivyokuwa awali. Kushoto ni Mkurugenzi wa Uendeshaji, Anselim Peter na Dk. Abdulsalaam Omar Mkurugenzi wa Huduma za Tiba.

# Vijiji 57 vyakosa maji Masasi

**Na Hamisi Nasri,** MASASI

VIJIJI 57 viliyoko wilayani Masasi mkoani Mtwara havina huduma ya majisafi na salama, hali inayosababisha wakazi wake kutembea kuyafuata umbali mrefu.

Hayo yalielezwa mjini Masasi na Meneja wa Wakala wa Maji na Usafi wa Mazingira Vijijini (RUWASA), Juma Yahaya, alipokuwa akipokea shehena ya mabomba ya maji yenye urefu wa kilomita 40 kutoka Wizara ya Maji.

Wizara ilitoa mabomba hayo kutatua kikwazo cha maji wilayani Masasi katika majimbo ya Masasi Mjini, Ndanda na Lulindi.

Alisema hadi kufikia Julai, jumla ya vijiji 57 katika wilaya hiyo havijapatiwa huduma ya majisafi na salama, huku serikali ikiendelea kuweka mikakati ya kuhakikisha vijiji hivyo vinapata huduma hiyo.

Alisema kutokana na miradi mbalimbali ya maji inayoendelea kutekelezwa wilayani Masasi, na kwamba hadi Septemba 2021, vijiji 17 viko katika mkakati ya serikali kupatiwa huduma ya majisafi na salama, hivyo vitabakia vijiji 40.

Akizungumza katika makabidhiano ya mabomba ya maji, Mkuu wa Wilaya ya Masasi, Claudia Kitta, aliipongeza wizara kwa kutoa mabomba, na kwamba serikali ya wilaya itahakikisha inasimamia vema ili huduma ya maji ipatikane kwa vijiji vilivyosalia.

Mbunge wa Masasi, Geoffrey Mwambe, alisema baada ya kupatikana mabomba, fedha zingine zinazotarajia kupatikana, zitamaliza kabisa kikwazo cha maji Masasi na wananchi wataanza kupata huduma ya majisafi na salama.

# Simbachawene ashtukia kero magendo mipakani

**Na Felix Mwagara**

WAZIRI wa Mambo ya Ndani ya Nchi, George Simbachawene, amesema serikali itavidhibiti vipenyo zaidi ya 300 vilivyopo katika mpaka wa Tanzania na Kenya, maeneo ya Holili na Tarakea wilayani Rombo, Mkoa wa Kilimanjaro. Amesema uwapo wa vipenyo hivyo umesababisha serikali kupoteza mapato mengi kwa sababu wanaopitisha magendo hutumia njia hizo kupitisha bidhaa mbalimbali kutoka upande mmoja kwenda mwingine.

Waziri Simbachawene alisema hayo katika kikao na maofisa wa taasisi mbalimbali wanaofanya kazi katika mipaka hiyo, baada ya kumaliza kukagua na kusikiliza taarifa zao kutoka kwa taasisi zote katika mipaka hiyo.

"Hili jambo halikubaliki, lazima lifanyiwe kazi, nimelipokea ila naomba mjue kuwa kati ya mambo ya msingi kama nchi ni kudhibiti mipaka, huwezi kuwa na nchi halafu watu wanaingia na kutoka wanavyotaka, haiwezekani, lazima nikae na mawaziri wenzangu pamoja na makatibu wakuu tuone jambo hili tunalidhibiti vipi," alisema Simbachawene.

Aliongeza kuwa uwapo wa vipenyo zaidi ya 300, ni vingi sana, hivyo ni lazima vidhibitiwe kwa kuharibiwa kwa sababu serikali inapoteza mapato mengi na kamwe jambo hilo halitapuuzwa.

"Suala hili ni la msingi katika maendeleo ya nchi, hivyo siwezi kufanya maamuzi peke yangu, naomba niseme kuwa hii taarifa nimeipokea, na nitaipeleka kwa viongozi ili tuone tunafanyaje katika kudhibiti hivi vipenyo, ili watu wapite katika njia halali na zinazoeleweka, na kwa hatua hiyo serikali iweze kupata mapato," alisema Simbachawene.

Mfawidhi wa Uhamiaji Kituo cha Holili, Eliaichi Marandu, alimwambia Simbachawene kuwa mpaka huo unakabiliwa na changamoto ya uwapo wa vipenyo vingi visivyo rasmi, hali ambayo inawafanya kushindwa kudhibiti suala la magendo mpakani licha ya kuwa wanajitahidi mara kwa mara kufanya doria.

"Mheshimiwa Waziri, vipenyo hivi ambavyo vipo katika maeneo mbalimbali, yakiwamo ya Kamwanga, Rongai hadi mpaka wa Holili, vipo zaidi ya 300 na ni vikubwa hata magari makubwa yanaweza kupishana, hivyo kuwapo na vipenyo kuna kuwa vigumu kudhibiti licha ya kuwa tunajitahidi kufanya doria," alisema Eliaichi.

Hata hivyo, upande wa mpaka wa Tarakea wamevuka kiwango cha ukusanyaji wa mapato ambapo kuanzia mwezi Julai mwaka 2020, kituo cha Tarakea kilitarajiwa kukusanya shilingi bilioni 13.

Juni mwaka huu 2021, kituo hicho kilikusanya zaidi ya shilingi bilioni 15.




Maclina Romward Rugeiyamu (kulia) mkazi wa Bukoba mkoani Kagera akifurahia zawadi ya Power Tiller aliyojishindia kupitia promosheni inayoendelea ya bia ya Balimi, baada ya kukabidhiwa na meneja wa bia hiyo, Pamela Kikuli (katikati). Hafla ya makabidhiano ilifanyika mjini Bukoba mwishoni mwa wiki. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Timu ya RC kuchunguza wizi wa dawa

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Mkoa wa Morogoro, Martine Shigela, amesema ataunda timu maalum ili kuchunguza upotevu wa dawa zinazotolewa na serikali, huku akiwaonya watumishi wa umma wasiokuwa waaminifu kubadilika.

Shigela aliyasema hayo wilayani Kilosa, alielezea kusikitishwa na upotevu wa dawa ambazo hutolewa na serikali kwa ajili ya kutoa kuduma ya matibabu kwa wananchi.

"Nitaunda timu maalum kuchunguza watumishi wa serikali wote wanaojihusisha na wizi wa dawa ili hatua kali za kinidhamu kwa wote watakaobainika hatua zichukuliwe kwani wanatuhujumu," alisema Shigela.

Alisema haiingili akilini kuona fedha zinaletwa na serikali vituo vya kutolea dawa, lakini wananchi hawapati dawa kutokana na baadhi ya watumishi wa serikili wasiyo waaminifu kuamua kuiba dawa hizo.

Shigela alisema jambo hilo kamwe hawezi kulivumilia katika kipindi chake cha ukuu wa mkoa wa Morogoro, hivyo atahakikisha wote wanaojihusisha na wizi wanachukuliwa hatua za kisheria ili iwe fundisho kwa watumishi wengine.

"Serikali yetu imekuwa ikituletea fedha kwa ajili ya kununulia dawa, lakini baada ya siku mbili tu dawa hizo zote zinakuwa zimeisha, huu ni uhuni mkubwa," alisema Shigela.

Alieleza serikali imekuwa ikifanya kila liwezekanalo kutatua changamoto ya huduma ya afya kwa kujenga vituo vya afya, zahanati na hospitali kila wilaya na mikoa, lakini baadhi ya watu wanakwamisha juhudi hizo.

Shigela alisema ataunda timu ambayo itapita katika zahanati, vituo vyote vya afya pamoja hospitali zote za mkoa huo itakayokuwa na kazi ya kuchunguza mtandao wote wa wizi huo.

Mkazi wa Kilosa, Majambaa alipongeza kauli hiyo kwamba baada ya timu hiyo kuundwa, watakuwa mstari wa mbele kuhakikisha mtandao huo wa wezi unapatikana.

Abel Lucas, alisema mkoa huo kwa sasa unakabiliwa na changamoto ya upotevu wa dawa, hali ambayo imekuwa ikiwaathiri sana wananchi wanaokwenda vituo vya afya kutafuta matibabu.

# Serikali yaisaidia shule iliyoungua Muleba

**Na Lilian Lugakingira,** MULEBA

SHULE ya Sekondari ya Seminari ya Kiislamu ya Jakaya Kikwete iliyoko wilayani Muleba mkoani Kagera, ambayo mabweni yake mawili yanayotumiwa na wanafunzi wa kike kuungua na kusababisha hasara, imepatiwa msaada.

Moto huo ulisababisha uharibifu wa majengo na vifaa vya wanafunzi mwishoni mwa wiki.

Msaada uliotolewa na serikali ni wa vifaa vya ujenzi na vya shule vyenye thamani ya shilingi milioni kumi.

Akikabidhi vifaa hivyo ambavyo ni mifuko ya saruji 170, magodoro 43, mashuka 87, madaftari makubwa na madogo 600, sare za shule na mabegi ya kuhifadhia nguo, Mkuu wa Wilaya ya Muleba, Toba Nguvila, alisema serikali imefikia uamuzi wa kutoa msaada wa vifaa hivyo ili kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo bila usumbufu.

Nguvila aliwataka wanafunzi wa shule hiyo ambao vifaa vyao vimeungua kutokata tamaa badala yake waendelee kusoma kwa bidii ili kufaulu mitihani na kutimiza malengo yao ya baadae, na kwamba serikali inaendelea kutafuta misaada zaidi kuhakikisha mabweni yote yanarejeshwa katika hali ya kawaida.

"Nina uhakika mtaendelea kusomea katika mazingira mazuri, hivi vitu tumevitafuta ili viwasaidie, rai kwenu uongozi wa shule anzeni kurekebisha mabweni haraka, ili watoto hawa waendelee kupata mahala pa kulala," alisema. Naye Ofisa Elimu Sekondari wa wilaya hiyo, Jered Muhile, aliwataka wanafunzi hao kuwa na subira wakati serikali ikiendelea kufanya jitihada za kudhibiti majanga kama hayo yasitokee tena.

"Walimu tumekwishaongea nao na kuwaweka sawa kisaikolojia na tunafahamu hawa wanafunzi wameunguliwa mali zao wakawa na taharuki, pia nao tumekaa na kuzungumza nao na kuwarudisha katika hali ya kawaida, hiyo wako tayari kuendelea na masomo, wakati mapungufu mengine yakiendelea kufanyiwa kazi," alisema Muhile.

Mkuu wa shule hiyo, Yasin Mikidad, aliishukuru serikali kwa msaada huo unaolenga kuwawezesha wanafunzi kuendelea na masomo kwa wakati na kuwasihi wanafunzi kuendelea kuwa wavumilivu katika kipindi hiki ambacho uongozi wa shule na serikali wanaendelea kutafuta misaada kwa ajili yao.

Mmoja wa wanafunzi, Husna Suleiman, alisema wamepoteza vifaa vyao zikiwamo nguo, madaftari na vitabu, hali inayoweza kuchangia kurudi nyuma kimasomo, na kuomba kuendelea kusaidiwa.

Mabweni mawili yenye wanafunzi 138 wa kuanzia kidato cha kwanza hadi cha nne, yaliteketea kwa moto Julai 23, mwaka huu, majira ya mchana wakati wanafunzi hao wakiendelea na somo la dini ya Kiislamu.

Nipashe
# TESA
Jumanne Julai 27, 2021
TEKNOLOJIA · ELIMU · SAYANSI



## Ujenzi shule za wanasayansi mabinti usisahau kuwaandaa
Ukurasa 13



Ukurasa 12
### Ndivyo TANAPA inavyopika maelfu ya mabalozi utalii



Ukurasa 14
### Ulazimishaji huu sarufi unawakera watumiaji wasanifu wasijitutumue

ELIMU
NA SABATO KASIKA

# Shule zilivyoamka kutekeleza mwongozo wa kuikabili corona

BAADA ya serikali kutoa mwongozo wa udhibiti wa maambukizi ya corona shuleni, vyuoni na taasisi za elimu, kulinda wanafunzi, walimu na wafanyakazi baadhi ya shule zimeanza kuchukua hatua wakati nyingine zinasuasua.

Miongoni wa shule hizo zinazotimiza wajibu kikamilifu ni za binafsi ambazo zina maji tiririka na sabuni, kutumia barakoa na miundombinu ya kunawa ikiwa imekamilika, mathalani zipo baadhi ya shule kama Mbezi High School na Green Belt wanafunzi huanza kunawa getini na wakishaingia ndani husafisha tena mikono ili kwenda madarasani.

Mbezi High School na Azania ni mfano ambako pamoja na maji kadhalika kuna vitakasa mikono, vyote vikipatikana kwenye 'mageti' na pia maji hayo yapo nje ya milango ya madarasa ambapo wanafunzi hunawa kabla ya kuingia madarasani, huku kila mmoja akiwa amevaa barakoa.

Uchunguzi uliofanywa na Nipashe, umegundua kuwa hatua hiyo inakwenda sambamba na wanafunzi madarasani kukaa kwa kupeana nafasi kama njia mojawapo ya kuepusha maambukizi na kuwaweka salama wanapokuwa shuleni.

Kimara sekondari ni miongoni mwa shule hizo, maji tiririka na vitakasa mikono kwa ajili ya wanafunzi, vimewekwa nje ya milango ya kuingia madarasani na kila mmoja ajitahidi kuna kwanza kabla ya kuingia kuanza masomo, huku wakiwa wamevaa barakoa.

Changamoto zinazoibuka katika shule nyingi za serikali ni za msingi na sekondari ni baadhi kukosa uzio, hivyo kuvuruga utaratibu wa wanafunzi kuingia kwenye mlango mkuu na kunawa mikono kwa maji tiririka kabla ya kuingia shuleni.



Katibu Mkuu Wizara ya Afya, Profesa Abel Makubi (kushoto), ndiye aliyetoa mwongozo wa kudhibiti corona shuleni na kote nchini. Ni wakati wa Wizara kuweka utaratibu wa kufuatilia utekelezaji. **PICHA: MAKTABA**

Walimu wanasema kuwepo uzio kungesaidia wanafunzi kuingia kupitia sehemu moja, kunawa kabla ya kuingia darasani, kutumia vitakasa mikono na kutumia barakoa.

Hata hivyo katika shule hizo, wanafunzi na wafanyakazi wengine wanaotumia njia mbalimbali za kuingilia shuleni wanavaa barakoa, huku walimu wakinawa maji tiririka na kutumia vitakasa mikono huduma zinazopatikana nje ya ofisi zao.

### UTOAJI MSAADA

Mwongozo pia unataka walimu wa afya kupewa elimu ya utoaji wa msaada wa kisaikolojia kwa ajili ya kusaidia wanafunzi, walimu pamoja na wafanyakazi katika kupambana na kudhibiti ugonjwa huo.

Mbali na hilo, uongozi wa shule, vyuo na taasisi za bweni unatakiwa kuweka nafasi ya kutosha (mita moja) kati ya kitanda kimoja hadi kingine na kudhibiti uchangiaji wa vifaa kwa wanafunzi kama vile taulo, mashuka, vyombo vya kuogea na vifaa vya usafi wa mwili.

Hata hivyo, huenda suala la kudhibiti vifaa vya kuogea huenda likawa gumu kwenye shule za bweni kwa kuwa zipo baadhi hazina maji ya bomba yanayotolewa na mamlaka za umma mbali na yale ya kuchimba na kusukuma kwa umeme yanayodaiwa kuwa yana chumvi.

Vilevile, mwongozo huo unaelekeza uongozi wa shule, vyuo na taasisi viweke utaratibu bora wa upatikanaji wa barakoa katika maeneo yao kwa gharama nafuu, huku wazazi na walezi wakitakiwa kuhamasishwa kuwapa watoto wao barakoa. Walimu na wafanyakazi wote katika shule, vyuo na taasisi za elimu, wanatakiwa kuvaa barakoa muda wote wa kazi, huku watoto wenye umri chini ya miaka mitano na wenye magonjwa ya moyo, selimundu (sickle cell) mfumo wa hewa kama vile pumu na matatizo mengine wasizivae.

Uongozi wa vyuo na shule pia unatakiwa kuhakikisha uwepo wa vifaa vya kuhifadhia taka zitokanazo na barakoa zilizotumika na kuziteketeza kama taka nyingine hatarishi ili kuzuia maambukizi ya virusi vya corona.

Katika eneo hilo, baadhi ya shule zilizotembelewa ikiwamo Green Belt na Mbezi High School, kuna mapipa ya taka maalumu ya kuwekea barako hizo hasa zile ambazo si za vitambaa na pia zimeweka mashimo ya takataka ya kuzichoma na kuziharibu.

### CORONA SHULENI

Kwa wanafunzi ambao watakaobainika kuwa na dalili za corona wakiwa shuleni na vyuoni, uongozi unatakiwa kutoa taarifa kwenye kituo cha huduma kilichoko karibu na kumpeleka kwenye kituo husika kwa uchunguzi na matibabu.

Aidha, mwongozo unataka usafiri wa kwenda na kurudi shule na chuo, wamiliki wa magari wahakikishe abiria na wahudumu wote wanavaa barakoa na kutumia vitakasa mikono kabla ya kupanda na wakati wa kushuka.

Pamoja na kuvaa barakoa, wamiliki wa mabasi ya shule wanatakiwa kuweka vitakasa mikono kwenye mabasi kwa ajili ya wanafunzi wakati wa kupanda na kushuka.

Kwenye suala la mazingira ya kujifunzia, mwongozo unataka uongozi wa shule na vyuo kuzingatia kuwa watumishi wote na wanafunzi wanakaa kwa umbali usiopungua mita moja kati ya mtu mmoja na mwingine wawapo sehemu yoyote wakati wa mafunzo.

Shule na vyuo vyenye wanafunzi wengi, mwongozo unautaka uongozi kuweka utaratibu wa wanafunzi kuingia madarasani kwa awamu, huku walezi wa mabweni wakitakiwa kupewa mafunzo na namna ya kubaini ishara na mabadiliko ya mwanafunzi, pia wafanye ukaguzi mara kwa mara kwa mabwenini na afya za wanafunzi.

ELIMU

NA ALPHONCE KABILONDO, GEITA

# Ndivyo TANAPA inavyopika maelfu ya mabalozi utalii



Hifadhi ya Bonde la Ngorongoro ni moja ya maajabu ya dunia yanayovutia wataliii wengi. **PICHA: MTANDAO**

TANZANIA imesheheni vivutio vingi vya utalii na ipo juu kwenye chati kutokana na kuwapo hifadhi nyingi za taifa, mito, Mlima Kilimanjaro, maziwa kadhaa na pia uwepo wa Bonde la Ngorongoro, wanamoishi binadamu na wanyamapori.

Utalii unachangia zaidi ya asilimia 17 ya pato la taifa na asilimia 25 ya fedha za kigeni zinazoingizwa nchini kupitia watalii wa ndani na nje.

Tanzania ina hifadhi za taifa 22 zinazosimamiwa na Shirika la Hifadhi za Taifa (TANAPA) ikiwa ni sekta inayotoa ajira kwa watu takribani milioni ya 5.5 kwa mwaka ni kwa mujibu wa Kamishna Msaidizi Kitengo cha Uhifadhi na Uhusiano wa Jamii (TANAPA), Godwell Meng'ataki.

Akizungumza katika mahojiano na Nipashe anasema lakini changamoto ni ufahamu wa hifadhi na ulinzi wa rasilimali hizo.

Anaongeza kuwa kuanzia sasa juhudi zinafanywa ili kuwa na mabalozi bora wa kuutangaza utalii na kutambua umuhimu wa hifadhi za taifa.

"Ili kutimiza azma hiyo tumeanza kutoa elimu kwa walimu wa masomo ya Jiografia, wakuu wa shule za msingi na sekondari,

> "Kwa kipindi cha Machi hadi Juni 2021 elimu imefika katika mikoa 10, wilaya 16 na vijiji 66 lengo ni kufikia shule zote zilizopo jirani na hifadhi zote 22, anasema Meng'ataki.

maofisa elimu kata, wilaya pamoja na wakurugenzi watendaji wa halmashauri kwenye wilaya na mikoa yenye hifadhi."

Anabainisha kuwa kutokana na Watanzania wengi kutokuwa na elimu ya uhifadhi wa hifadhi za taifa hususani wanafunzi na vijana imewasukuma kutoa elimu hiyo kwa makundi hayo.

"Kwa kipindi cha Machi hadi Juni 2021 elimu imefika katika mikoa 10, wilaya 16 na vijiji 66 lengo ni kufikia shule zote zilizopo jirani na hifadhi zote 22, anasema Meng'ataki.

Aidha, katika muda huo, anasema wanafunzi 5,500 wa sekondari na 9,696 wa msingi wa shule zilizo jirani na hifadhi 10 kati ya 22 zilizo chini ya TANAPA wamepatiwa elimu hiyo.

Kadhalika, kamishna huyo anakiri kuwa changamoto ya wananchi kuvamia hifadhi na kuanzisha shughuli za kilimo na makazi na uwindaji haramu kwenye baadhi ya hifadhi imekuwa ikichangia wanyama adhimu kutoweka na kupungua kwenye hifadhi na kusababisha sekta hiyo kukosa mapato.

Kamishna huyo anabainisha kuwa hifadhi hizo ni rasilimali za Watanzania wote hadi vizazi vilivyopo na vijavyo ndiyo maana wameanza na juhudi hizo ili kuzitunza na kudhibiti uharibifu na uvamizi wa hifadhi ili vizazi vijavyo vinufaike na rasilimali hizo.

Kuna changamoto kubwa tena kuna baadhi ya wanafunzi hawawezi hata kuonyesha hifadhi za taifa kwenye ramani, anasema mtaalamu huyo.

"Tumeanza kwa majaribio kutoa elimu hiyo kwenye mikoa na wilaya zenye hifadhi lengo ni kuwatengeneza mabalozi utalii na kutambua uhifadhi mtaala huo ukiingizwa kwa shule za msingi na sekondari na kuboreshwa zaidi, anasema kamishna huyo.

Mhifadhi Mkuu Kanda ya Magharibi Martin Loiboki, anasema kutokana na wananchi kutotambua sheria na elimu ya uhifadhi wamekuwa wakivamia baadhi ya maeneo ya hifadhi na kuibua migogoro kati yao na hifadhi.

"Pia kuna baadhi wamekuwa wakihangaika kuomba kibali kwenda kwenye hifadhi pasipo kujua sheria kuwa ni marufuku kuwinda wanyama maeneo hayo."

"Ni marufuku hakuna kibali kinachoruhusu kwenda kuwinda wanyama kwenye hifadhi za taifa sheria iko wazi inaeleza," anasema Loiboki.

Anasema elimu shuleni na kwa viongozi ni muhimu ili wanafunzi na jamii iwe na ufahamu na kwamba wameanza majaribio kwa kutoa elimu hiyo kwa wanafunzi wa shule za msingi na sekondari jirani wa hifadhi.

"Wanafunzi hawa ndiyo viongozi wa baadaye hivyo wasipotambua elimu ya uhifadhi kwa mapana hawatambua umuhimu wa uhifadhi pamoja na utalii tunakusudia somo hilo kuwekwa kwenye mtaala wa elimu," anasema mhifadhi huyo.

Mhifadhi huyo anasema kuwa baadhi ya hifadhi zinazopatikana katika Kanda ya Magharibi ni Serengeti ambayo imegawanywa katika mikoa ya Mara, Arusha na Simuyu, Kisiwa cha Rubondo na Burigi Chato mkoani Geita, Kisiwa cha Sanane - Mwanza na Mto Igala Ibanda na Rumanyika.

**ELIMU NI ULINZI**

Mkurugenzi wa Halmashauri ya Wilaya ya Chato, Eliudi Mwaiteleke, mmoja wa wakurugenzi watendaji waliopata elimu ya uhifadhi anasema anatamani elimu hiyo kutolewa kwa wanafunzi wa darasa la tatu ili watakapohitimu wawe na uelewa mpana kwenye uhifadhi wa hifadhi za taifa na utalii.

Mwaiteleke anasema kutokana na uwepo wa hifidhi ya Burigi Chato na Kisiwa cha Rubondo katika halmashauri hiyo uchumi unategemwa kuwa utapaa kupitia makusanyo kufuatia mpango wa elimu inayotolewa na TANAPA.

Ofisa Elimu Kata ya Izumacheli Wilaya ya Geita, mkoani humo Tommy Samson, anasema kuwa elimu ya uhifadhi itawasaidia wanafunzi kufahamu ulinzi wa rasilimali za taifa na kutambua umuhimu wa utalii.

"Mkakati huu ni mzuri na wa kuwajenga walimu na wanafunzi wasio na uelewa kwa kuwa mpaka sasa wanatambua kuwa watalii ni wageni kutoka nje pekee lakini kumbe wapo watalii wa ndani ambao ni wengi pia."

Mwalimu Meckitlida Gendo , anasema kuwa somo hilo limekuwa likifundishwa tangu awali lakini halikupewa kipaumbele kama somo la mazingira na TANAPA imekuja na mpango bora kwa elimu wa kuwafundisha walimu, wanafunzi pamoja na kuhamasisha utalii wa ndani.

Mkuu wa Wilaya ya Geita, Wilison Shimo, anasema dunia inakumbwa na mabadiliko ya tabianchi bila kuweka udhibiti katika uharibifu wa mazingira ya hifadhi kuna hatari ya kupata madhara makubwa kama ukame, maji kukauka, na mmomonyoko wa udongo.

"Ni ukweli usiopingika kuwa bila kuchukua hatua upo uwezekano mkubwa wakupatwa na athari kimazingira na wanyama kutoweka hivyo kila mmoja kwa nafasi yake ana jukumu la kupambana na uharibifu wa mazingira na wavamizi wa hifadhi."

Kuhusu mpango maalumu wa kuwaanda mabalozi wa utalii unaofanywa na TANAPA anasema walimu hasa wanaofundisha Jiografia wanatakiwa kuchukulia uzito mafunzo ya elimu hiyo.

ELIMU

**NA GAUDENSIA MNGUMI**

# Ujenzi shule za wanasayansi mabinti usisahau kuwaandaa



Wasichana wanasayansi wanahitaji kuandaliwa, kuhamasishwa na kupewa motisha ili mpango wa kuwa na shule maaluma kwa ajili yao uwe endelevu. **PICHA: MTANDAO**

BAJETI ya serikali inayoanza kutumika mwezi huu, itaanza na kuweka jiwe la msingi la kujenga sekondari maalumu za wasichana za sayansi.

Rais Samia Suluhu Hassan, ndiye anayetoa hakikisho hilo wakati akizungumza na kinamama wa mkoa wa Dodoma na kuahidi kuwa, Tanzania imeazimia kupunguza pengo la ufahamu wa masuala ya kisayansi na kiteknolojia kati ya wanawake na wanaume.

Anasema tofauti ya uelewa wa masuala ya kisayansi na kidijitali miongoni mwa wasichana na wavulana anayaona nyumbani kwake. Anatoa mfano wa wajukuu wake Ibra na Samia, anasema, simu yake inapokorofisha akashindwa kuiweka sawa, anayeirekebisha ni Ibra.

Anaeleza kuwa akimweleza Samia, anasema kuwa hawezi na anakimbilia kwa kaka yake anayemaliza tatizo hilo na kuiweka sawa, maelezo hayo yalikuwa yanabainisha tofauti iliyoko kati ya wanawake na wanaume kwenye masuala ya sayansi na teknolojia ya kidijitali inayotawala dunia sasa.

Ndipo Rais anapoahidi kuwa serikali itaanza kujenga shule hizo kwa kila mkoa ili kuondoa pengo hilo na kazi hiyo ingeanza mwezi huu.

Serikali inapoanza ujenzi wa shule kinachokwenda pamoja na juhudi hizi ni mikakati ya kuwaandaa na kuwapata wasichana.

Wasichana au mabinti wanaopenda kusoma sayansi kuanzia katika hatua za awali ili mpango huo uwe endelevu na wenye tija.

"Kila mkoa, hata wilaya kuwe na shule za wanafunzi wenye vipaji maalumu kuanzia msingi hadi sekondari. Siyo lazima tuwasubiri wakienda sekondari hasha, tuanze kuwaanda tangu awali," anasema Profesa Davis Mwamfupe.

Profesa Mwamfupe anaeleza hayo anapoulizwa na Nipashe, mambo muhimu wakati wa maandalizi ya kuwapata wanafunzi wa kuingia kwenye sekondari za sayansi maalumu kwa wasichana.

Profesa Mwamfupe, ambaye ni mwalimu kitaaluma akifundisha vyuo vikuu vya Dar es Salaam na Dodoma, anasema ili shule hizo ziwe endelevu kuanzia sasa hatua za kusaka na kusuka wasichana wenye vipaji maalumu zianzie kwa kuweka mikakati ikiwa ni pamoja na kuwa na shule zenye vipaji maalumu.

Lakini ana angalizo: "Siyo lazima waende sekondari. Wanaweza kuanzisha na kuendeleza ubunifu na ugunduzi wao kwenye vyuo vya mafunzo ya ufundi," anasema.

Anaongeza kuwa katika hatua hiyo, wanaofanya vizuri na kuboresha kazi zao watakuwa na nafasi ya kubuni, kutafiti zaidi na kuwa kazi bora za kisayansi na teknolojia chini ya waangalizi na wasaidizi mahiri.

Anasema Tanzania ya leo inahitaji zaidi vyuo vya mafunzo ya ufundi (VETA) kwa ajili ya kuwaandaa na kuwapika vijana wabunifu na wagunduzi kwenda mbele kwenye vyuo vya kati na vikuu.

> "Kama walivyoweza wanawake wengine, hata wao wanaweza tena hata zaidi yao. Wanafunzi wa kike wasisitizwe kuwa wao ni sehemu muhimu katika kufanikisha maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini." Anasema Lumbagala.

Hata hivyo, anakumbusha kuwa vyuo vya VETA ndiko kunakozalishwa ajira na kwamba ni eneo vijana wanapojifunza mambo mengi kama uzalishaji kwenye kilimo, uvuvi, ufugaji, ufundi wa aina mbalimbali, kazi za viwandani na usindikaji.

Anashauri kuwa pamoja na kuwaandaa mabinti kwenda kwenye shule maalumu za sayansi na vyema pia wataalamu wa sayansi na teknolojia waanze kuwafuatilia katika ngazi za chini ili kuibua wabunifu na wagunduzi wenye vipaji maalumu na kuwajengea msingi na mazingira ya kuendeleza vipaji vyao.

**WALIMU WA SAYANSI WANAWAKE**

Mwalimu Reuben Lumbagala anayefundisha Sekondari ya Mlali mkoani Dodoma, anashauri kuwa ili kuwa na mafanikio katika mpango huo, wasichana wajengewe uwezo wa kujiamini kwanza kuwa wanaweza kumudu masomo hayo.

"Wasichana kwanza wahamasishwe kuwa wana uwezo mkubwa wa kuyamudu masomo ya sayansi. Pia kuwe na mpango wa kuandaa na kuwaajiri walimu wa sayansi wa kike wa kutosha shuleni."

Anasema pamoja na kuwapo walimu hao, wawepo wana taaluma za sayansi kama wauguzi, madaktari na wahandisi wanawake kwenye mkakati wa kuwaandaa wasichana kupenda sayansi kwenye shule hizo ili iwe chachu ya kuwahamasisha kuyapenda masomo hayo.

"Kama walivyoweza wanawake wengine, hata wao wanaweza tena hata zaidi yao. Wanafunzi wa kike wasisitizwe kuwa wao ni sehemu muhimu katika kufanikisha maendeleo ya sayansi na teknolojia nchini." Anasema Lumbagala.

Mahitaji ya wanasayansi kwa Tanzania ni makubwa na wanawahitaji wanawake na wanaume kwa pamoja, hivyo wasichana wasome kwa bidii wakijua wana umuhimu kwenye ujenzi wa nchi yao, anasema mwalimu huyo.

**MOTISHA**

Mwalimu Lumbagala anataja motisha kwa wanafunzi wa kike wanaofanya vizuri katika masomo ya sayansi kuwa ni jambo la muhimu kufanikisha mkakati huo.

Katika ngazi za halmashauri, pawepo na motisha kwa wanafunzi wanaofanya vizuri kwenye sayansi kuanzia shule za msingi, kidato cha pili hadi nne ili kuongeza hamasa ya kuipenda zaidi.

Anaamini kuwa motisha kwa wanafunzi hao itaongeza ari kwa wasichana kusoma na kujiendeleza kwenye sayansi ili kupata wataalamu wa kutosha kwenye eneo hilo na kupunguza pengo la uelewa baina ya wanawake na wanaume.

"Motisha hapa ni pamoja na kulipiwa ada kwa mwaka mmoja na kugharamiwa mahitaji kama kompyuta. Mabinti wanasayansi wapewe nafasi za kuzuru viwandani, maabara na kufanyakazi kwa muda kama sehemu ya mafunzo." Anashauri.

ELIMU

NA MICHAEL ENEZA

# Ulazimishaji huu sarufi unawakera watumiaji wasanifu wasijitutumue



Wadau wakijichagulia vitabu vya Kiswahili katika duka lililoko Chuo Kikuu cha Dar es Salaam.: **PICHA MTANDAO.**

JITIHADA za kuendeleza matumizi ya Kiswahili katika nyanja tofauti za maisha na uchumi kwa jumla zinaendana na juhudi za taasisi zinazohusika na kukua kwa lugha kutoa mwanga pale ambapo kuna hitilafu katika matumizi ya lugha.

Kwa mfano kupatikana kwa neno pale ambapo hitaji lipo mathalani, 'mask' wakati huu wa corona jina lililoibuliwa ni 'barakoa'.

Jitihada hizo za kitaasisi kujenga lugha zimewezesha maeneo mengi kupatikana kwa mifumo ya kujieleza ambayo labda ingechukua muda kujijenga yenyewe miongoni mwa watu, au isingekuwapo.

Hata hivyo, mara nyingi jitihada hizo hazielekei kujaza pengo halisi ila kulijaza kwa lafudhi ya Kiswahili.

Hapo ndipo unazuka utatanishi kuhusu matumizi ya misemo tofauti kama ni Kiswahili sanifu, au ni 'Kiswahili gani na kuna baadhi ya wataalamu wa Kiswahili wameanza kukosoa baadhi ya matumizi katika lugha ya kawaida kuwa ni mifumo ya kuongea Kiingereza na haifuatani na sarufi ya Kiswahili.

Tatizo hapo ni kuwa watu wakishaanza kuwasiliana au kuzungumza kwa mfumo fulani unaoeleweka, hakuna anayeweza kuja kama mtaalamu akaanza kufundisha kitu kingine.

Ni kwa sababu lugha zinatokana na mifumo ya nasibu hutokea bila kutazamiwa au kuzuka kwa bahati.

Inakuwa kana kwamba wanahitaji kufaulu mtihani wakati sivyo, au waongee Kiswahili kinachofurahisha wataalamu au kundi fulani.

> Tatizo hapo ni kuwa watu wakishaanza kuwasiliana au kuzungumza kwa mfumo fulani unaoeleweka, hakuna anayeweza kuja kama mtaalamu akaanza kufundisha kitu kingine.

Wanafunzi wa shule za msingi na zaidi sekondari wanafahamu kitabu kinachoitwa 'Common Mistakes in English,' makosa yanayofanywa kila wakati katika kuongea Kiingereza, lakini pengine kwa Kiswahili si rahisi kuwa na kitabu kama hicho.

Yako maeneo kwa uhakika unaweza kusema kuwa ni 'common mistake,' ni kosa la kawaida linafanyika katika maongezi, halafu ziko sehemu nyingine ambako ni matumizi ya kawaida na siyo makosa ya kuainishwa kwa njia isiyopingika.

Kwa mfano katika mazungumzo redioni unasikia mwanamuziki akumbushie 'nyimbo hii' aliitunga katika mazingira gani.

Ni wazi kuwa umoja ungestahili kutumika hapo, ambao ni 'wimbo' badala ya 'nyimbo' lakini katika lugha hakuna amri au sheria ni wapi kuna majina au maneno yasiyotofautiana na wingi wake, na ni sehemu ipi tofauti inajitokeza.

Kwa mfano hakuna wingi kwa wanyama ng'ombe, kuku, mbuzi, kondoo au farasi wanaowataja wanabakia kusema 'wengi,' badala ya kubadilisha neno.

Kuku wengi, farasi wengi, lakini siyo kundi hilo tu la majina, kuna 'nyota' iwe ni moja au ziwe nyingi au anga nzima bado ni nyota.

Hivyo kuna uwezekano katika Kiswahili kuwa na mazoea ya kupuuza wingi au umoja, mradi tu neno liwe 'linatamkika,' na ndiyo huu usemi wa 'nyimbo hii' ambao sasa ni kama 'fashion.'

> Yako maeneo kwa uhakika unaweza kusema kuwa ni 'common mistake,' ni kosa la kawaida linafanyika katika maongezi, halafu ziko sehemu nyingine ambako ni matumizi ya kawaida na siyo makosa ya kuainishwa kwa njia isiyopingika.

Kuna eneo jingine ambalo haliwezi kuingizwa katika usanifu ila kuonekana katika matumizi ya lugha, hata kama wasanifu wa lugha wataona kama inatumika kwa makosa, kwa maana ya hisia ya kubania 'pumzi' katika kujieleza. Dhamira hapo inakuwa ni kupunguza makali ya kitu kinachozungumziwa, au kuainisha (kuweka mkazo wa aina fulani), ingawa inaonekana kubana kujieleza kwa hisia halisi inatokea mara nyingi zaidi.

Kwa mfano ni kawaida kusema 'naomba' sukari, wakati unanunua bidhaa hiyo, na hivyo 'huombi' ila ni kukwepa kusema 'lete,' 'nipe' au 'nataka,' kwa sababu za ustaarabu na upole ambayo ni sawa na 'adabu' kwa Kiswahili, licha ya kuwa 'kutaka' sukari dukani siyo 'kukosa adabu.'

Halafu kuna hisia miongoni mwa 'wanazuoni' wa Kiswahili au wasanifu ambazo kimsingi hutokana na jamii inayowazunguka, si kwa maana ya jamii pana ya Watanzania ila jamii finyu kwa mfano ya wakazi wa Kariakoo, au kundi la mtaani ambako mzungumzaji au msanifu, huyo anakuwapo mara kwa mara, na hata iwe familia anakoishi.

Kwa mfano mtaalamu mmoja ambaye lafidhi anasema 'lafudhi' kwa jinsi ulimi wake ulivyokuwa unasikika redioni ni mkazi wa maeneo ambako watu wa jamii ya Kiarabu ni wengi.

Anasema kutamka 'nachukua nafasi hii' ni kosa, ingekuwa 'natumia nafasi hii' suala ambalo halina uhakika kama ni ukosoaji sahihi na pia anadai kuwa 'nawaambieni' siyo sahihi ila 'nakuambieni,' mwelekeo ambao pia una utata kudai hayo ni matumizi sahihi zaidi ukiwa mbele za watu.

Hapo kuna maeneo mawili ya hisia yanayokinzana, kwanza ni eneo la matumizi ya adabu ukiwa mbele za watu, ambako 'nachukua nafasi hii' ina ladha nzuri zaidi ya 'natumia nafasi hii,' na kwa upande mwingine 'nawaambieni' inakubalika kihisia, kiadabu, wakati 'nakuambieni' ina shari ndani yake. Ndiyo maana mara kadhaa baadhi ya wadadisi wanaona kuwa wasanifu wangetafiti matumizi ya lugha na mapana yake, wakaandika kamusi za vina vya matumizi ya maneno, si kupania kuwa viranja wa lugha kuondoa 'Kiingereza' katika sarufi, wakati jambo hilo linatokana na matumizi ya kawaida.

Si uelewa wa Kiingereza, ila ni kweli yako maeneo ambako Kiingereza kilisaidia kufuma na kuunda lugha nyingine nyingi kwa jumla.





## Dodoma yasajili kaya 300,000 mazao biashara

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

MKUU wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka amesema mpaka sasa wamesajili kaya 300,000 ambazo zina uhakika wa kuendesha kilimo cha mazao ya biashara.

Akizungumza mwishoni mwa wiki Mtaka, alisema kila kaya katika mkoa huo inapaswa kusajiliwa ili ujue una wakulima wangapi na wanalima heka ngapi ili kuwasiliana na taasisi ya fedha.

"Sasa hivi tuko katika zoezi la kuendelea kusajili kaya, tunahitaji kujua tuna watu wangapi ambao wanalima kilimo cha mazao ya biashara kama alizeti, zabibu na ufuta," alisema Mtaka.

Mtaka alisema lengo lao ni kuona wakulima wanafanya kilimo chenye tija ambacho kitawaletea faida wao pamoja na taifa ikiwamo kuwasaidia wao kujiinua kiuchumi.

Alisema mkoa umepanga kuwasiliana na Wizara ya Ardhi kwa ajili ya kulima mashamba yenye sifa za kulima zao la zabibu.

Pia, alisema watafanya utaratibu huo ili kupata ardhi sahihi ambayo inafaa kuendesha kilimo hicho kwa kuwa kinavunwa misimu miwili.

Alibainisha kuwa wanafanya hivyo ili PASS Trust wajue kuna mashamba kadhaa ili kuona namna ambavyo watasaidia katika kilimo hicho kwa kushirikiana na taasisi za fedha.

"Tunawashukuru PASS kwa kuamua kutembelea katika mashamba ya zabibu

hapa jijini Dodoma, tunaamini kilimo hiki kitazidi kusonga mbele, na kilimo cha mazao ya kibiashara, kinalipa ndio maana wako mstari wa mbele kuhakikisha wanasimamia fursa za kilimo zinapotolewa na wadau mbalimbali," alisema.

Naye Mwenyekiti wa Bodi ya PASS Trust, Dk. Tausi Kida, alisema taasisi yao imejikita kwenye suala la kilimo ndio maana wanatembelea wakulima ili kuona kilimo wanachofanya.

Hata hivyo, aliwataka wakulima wa Mkoa wa Dodoma kutumia fursa mbalimbali zinazotolewa na taasisi hiyo ili kujiinua kiuchumi.

# Ewura yabaini wajanja wanaokwepa kulipa kodi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MAMLAKA ya Udhibiti wa Huduma za Nishati na Maji (EWURA), imebaini baadhi ya wafanyabiashara wasio waaminifu wakichanganya mafuta yaliyolipiwa na yasiyolipiwa kodi.

Meneja wa Mawasiliano na Uhusiano wa EWURA, Titus Kaguo, aliyasema hayo alipokuwa akizungumza na waandishi wa habari baada ya wasilisho la sekta ndogo ya mafuta alilotoa kwenye semina kwa Taasisi ya Maendeleo ya Viziwi Tanzania(TAWAVITA), jijini hapa.

Alisema huo ni uchakachuaji mpya wa mafuta ambao unachangia upotevu wa mapato ya serikali.

"Jukumu la EWURA ni kudhibiti ubora na usalama na tija ya watoa huduma na uchakachuaji wa mafuta ni changamoto kubwa hapa nchini, katika sekta ndogo ya mafuta kazi kubwa imefanyika ya kudhibiti uchakachuaji wa kuchanganya petroli au dizeli na mafuta ya taa, lakini sasa kumeibuka uchakachuaji wa kuchanganya mafuta yaliyolipiwa kodi na yasiyolipiwa," alisema.

Alisema mamlaka hiyo itahakikisha inaendelea kupambana na uchakachuaji huo ili kuhakikisha serikali inapata kodi yake stahili. Hata hivyo, alisema juhudi za EWURA za kupambana na tatizo la uchakachuaji wa mafuta zimesaidia kupunguza uchakachuaji kutoka asilimia 80 mwaka 2017 hadi kufikia asilimia nne mwaka 2020.

Alisema mafanikio hayo yametokana na uamuzi wa EWURA uliofanyika Septemba mwaka 2010 kwa kuanzisha programu ya kuweka vinasaba kwenye mafuta yanayotumika nchini ili kudhibiti ukwepaji kodi, uchakuzi na kuweka mazingira ya ushindani wa haki. Alisema kuwa takribani asilimia 50 ya mafuta yanayoingizwa nchini ni yanayokwenda nchi jirani.

Akizungumzia kuondoa hali ya uuzaji wa mafuta kwenye chupa na madumu hususani maeneo ya vijijini, alisema EWURA inashirikisha wadau mbalimbali kufanya utafiti wa mahitaji ya mafuta vijiji na kubuni kituo cha gharama nafuu muafaka kwa maeneo ya vijijini.

"Tunataka vijijini kuwa na vituo bora vyenye gharama nafuu vinavyoweza kugharimu kati ya Sh. milioni 22.3 hadi Sh. milioni 32.35, EWURA inadhibiti ubora wa miundombinu ya mafuta ili kulinda afya, usalama na mazingira," alisema.

Alisema mpaka sasa EWURA imechukua hatua za kuhamasisha ujenzi wa vituo vijijini na imeandaa masharti nafuu ili kuvutia wawekezaji kwenye maeneo hayo.



Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, akikabidhiwa Mwenge wa Uhuru na Mkuu wa Mkoa Singida, Bilinith Mahenge, wilayani Bahi, jijini Dodoma jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Watumishi watakiwa kuinua sekta muhimu

**Na Renatha Msungu,** DODOMA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Fatuma Mganga, amewataka watumishi wa umma mkoani humo kuhakikisha wanainua sekta ya elimu, afya na kilimo.

Dk. Mganga aliyasema hayo mwishoni mwa wiki katika kikao kazi cha viongozi watumishi wa mkoa huo chenye lengo la kujadili mustakabali wa maendeleo ya mkoa.

Alisema katika suala la elimu Dodoma ipo nyuma wakati ni makao makuu ya nchi.

"Dodoma kila kitu kinapatikana hususani bajeti ya fedha ambayo inatengwa na serikali katika kuendeleza sekta hizo, iweje Mkoa wa Dodoma ushindwe kufanya vizuri suala la elimu au afya," alisema.

Alisema watumishi wanapaswa kuondoka na lugha moja ya kuhakikisha wanakwenda kuinua suala la elimu katika maeneo wanayotoka, ili Dodoma iwe juu.

"Nawaomba watu muende kuvaa sura za kazi, acheni masihara kafanyeni kazi Dodoma ijulikane kwa kila kitu," alisema Dk. Mganga.

Kuhusu suala la kilimo, aliwataka wataalamu kusimamia kilimo cha zabibu ambacho kinastawi vizuri mkoani Dodoma na mavuno ni mara mbili.

Alisema hivi karibuni Waziri Mkuu alipokutana nao, aliwataka kuhakikisha zao la zabibu linakuwa la kimkakati kwa kuwa lina faida kwa wakulima.

Awali, Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Anthony Mtaka, alisema elimu ni moja ya vipaumbele vyake katika utendaji na kuwahimiza watumishi kusimamia hilo.

"Kila siku tumekuwa tukipiga kelele juu ya wanafunzi kuonekana wakizagaa mtaani badala ya kuwapo shuleni, anataka kuona Dodoma inakuwa juu katika suala la elimu na vitu vingine hivyo ni vema watumishi washikamane kuhakikisha mkoa unasonga mbele kielimu na kushika nafasi za juu katika mitihani ya kitaifa."

"Kikao hiki naomba kiende kuleta matunda mazuri kazini nahitaji kuona mnashirikiana katika kazi na sio kuleteana majungu kazini," alisema.



# Chunya wazuiwa kuchimba dhahabu kuepusha mgogoro

**Na Grace Mwakalinga,** CHUNYA

WAZIRI wa Madini, Dotto Biteko, amepiga marufuku wachimbaji wadogo wa madini katika kijiji cha Chalangwa wilayani Chunya kuchimba dhahabu katika Mlima Kaputa kutokana na mgogoro uliopo baina yao na mwekezaji anayemiliki leseni ya uchimbaji katika eneo hilo.

Mwezi Mei mwaka 2019, wananchi hao waliwahi kusimamisha msafara wa Rais, Hayati Dk. John Magufuli na kumpatia taarifa za uongo kuwa mwekezaji anayechimba katika mlima huo, anaendesha shughuli zake mahali penye mradi wa matangi ya maji na penye makuburi.

Maelezo hayo yalisababisha Dk. Magufuli kumwagiza waziri mwenye dhamana kufuta leseni ya mwekezaji huyo akiamini kuwa maelezo ya wananchi hayo ni ya kweli.

Hata hivyo, baadaye wazee wa kijiji hicho walikwenda Ofisi ya Mkuu wa Wilaya ya Chunya na kumweleza kuwa maelezo yaliyotolewa kwa Rais wakati ule hayakuwa ya kweli na sasa wanahitaji aletwe mwekezaji mwingine ili aendelee na uchimbaji wa madini katika Mlima Kaputa.

Kutokana na maelezo hayo, Waziri Biteko juzi alitembelea eneo hilo lenye mgogoro na kubaini kuwa matangi yaliyozungumzwa pamoja na makaburi yako mbali na eneo lenye leseni ya mwekezaji na kujiridhisha kuwa walitoa taarifa za uongo mbele ya rais.

Baada ya kujionea hali halisi, Waziri Biteko alikwenda kufanya mkutano wa hadhara na wananchi na ndipo walipokiri kusema uongo na kusema waliamua kutoa taarifa za uongo kwa sababu hawamtaki mwekezaji Joseph Mwazyele kwenye kijiji chao.

"Hatumtaki mwekezaji Mwazyele kwa sababu amekuwa akiwakamata na kuwapeleka polisi vijana wetu wanapokwenda kuokota mawe kwenye mgodi wake, lakini pia anamiliki bunduki ambayo anaweza kuitumia kutupiga risasi," alisema Michael Katembo.

Alisema baada ya Rais kuagiza leseni ya Mwazyele ifutwe anaamini mlima huo sasa ni mali ya wananchi ambao wanaweza kupata mwekezaji mwingine aendelee na uchimbaji katika mlima huo.

Akizungumza na wananchi hao, Waziri Biteko alisema baada ya Rais Hayati Magufuli kuagiza leseni ya mwekezaji huyo ifutwe, alikwenda kwenye mfumo kuangalia akakuta mwekezaji huyo alikuwa tayari ameshatoa maombi ya kutaka iongezewe muda.

Alisema kutokana na agizo la Rais aliamua kusitisha leseni hiyo isiongezewe muda ili kwanza afanye uchunguzi wa kile kilichosemwa na wananchi.

Alisema baada ya kufika katika eneo hilo alibaini maelezo ya wananchi hayakuwa ya kweli na badala yake wananchi wenyewe ambao wanaochimba madini mahali yalipo makaburi hayo.

Hata hivyo, alipowauliza kama wanahitaji madini yaendelee kuchimbwa katika mlima huo, wananchi hao walisema mwekezaji asichimbe ila wao ndio waendelee kuchimba.

"Suala lililosababisha tuzuie mwekezaji asiendelee kuchimba kwenye mlima huu ni taarifa zenu wananchi kwamba kuna matangi ya maji na makaburi, na wala sio tabia mbaya ya mwekezaji, hivyo katika mgogoro huu tusizungumzie mtu tuzungumzie suala lenyewe," alisema Biteko.

"Ikiwa tunamwondoa mwekezaji kwa sababu ya uwapo wa matangi ya maji na makaburi, nadhani sababu hizi hazijaondoka bado ziko pale pale, hivyo naagiza mwekezaji asiendelee kuchimba na ninyi wananchi pia ni marufuku kwenda kuchimba kwenye mlima huo mpaka hapo mtakapokaa pamoja na kuelewana ndipo tutoe maelekezo mengineyo," alisema Biteko.

Alimwagiza Mkuu wa Wilaya ya Chunya, Mayeka Simon, kusimamia eneo hilo kuhakikisha hakuna mtu yeyote anaendelea na shughuli za uchimbaji.

"Kama ninyi hamtaki kuchimba mmekalia majungu, yaacheni hayo madini ardhini maana hayaozi, watakuja watoto wetu wasiokuwa na madini watayachimba," alisema Biteko.




Baadhi ya watoto wakipita katika eneo la Sokoine jijini Mbeya, huku wakiwa wamejitwisha mizigo ya kuni wakipeleka sokoni mwishoni mwa wiki. **PICHA: NEBART MSOKWA**

# KKKT yaazimia kurudisha makao makuu Tukuyu

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

ZAIDI ya waumini 300 na baadhi ya wachungaji wa Kanisa la Kiinjili la Kilutheri Tanzania (KKKT), Dayosisi ya Konde wamekutana mjini Tukuyu na kufikia maazimio manne ikiwamo kurejesha makao makuu ya Dayosisi hiyo mjini Tukuyu.

Pia, wameomba serikali kuzuia mkutano mkuu wa dayosisi, mwaka huu wakidai kuwa mkutano huo uliondaliwa na Askofu Edward Mwaikali ni batili na unaweza kuhatarisha amani.

Mkutano huo maalum ulioitishwa juzi, ukiongozwa na wazee wa kanisa hilo, ulifanyika mjini Tukuyu ukiwa na ajenda moja ya kupinga makao makuu ya dayosisi hiyo kuhamishiwa jijini Mbeya kinyume na katiba yao.

Mchungaji wa Kanisa la KKKT Dayosisi ya Konde, Dk. Stephen Kimondo, alisema bado waumini na baadhi ya viongozi wanatambua makao makuu ya kanisa hilo yako mjini Tukuyu na kwamba sadaka na michango itaendelea kutolewa na washirika na kukusanywa kwenye maeneo yao.

Aidha, alisema kwa sasa hawana imani na Askofu Mwaikali pamoja na viongozi walioridhia makao makuu kuhamishiwa jijini Mbeya badala ya Tukuyu.

"Tunamtaka Askofu Mwaikali asijishughulishe na jambo lolote linalohusu Dayosisi mpaka hapo mkutano mkuu maalum utapoitishwa na kusimamia na mkuu wa kanisa akishirikiana na Msajili," alisema Mchungaji Dk. Kimondo.

Mwenyekiti wa mkutano huo, Stanton Mwambulukutu, alisema wameteua kamati ndogo ya kwenda kuonana na Mkuu wa Mkoa wa Mbeya, Juma Homera, kumwomba azuie kufanyika kwa mkutano mkuu wa dayosisi ya Konde ambao umeandaliwa na Askofu wa Dayosisi.

Miongoni mwa watumishi wa dayosisi hiyo akiwamo, Elizabeth Sekile, alisema kwa sasa uchumi wa makanisa umeyumba sadaka zote zinaenda kwenye makao ya dayosisi na kutafunwa na watu wachache.

# Jela miaka 4 kuua mpenzi wake bila kukusudia

**Na Grace Mwakalinga,** MBEYA

MAHAKAMA ya Hakimu Mkazi Mkoa wa Mbeya, imemhukumu kutumikia adhabu ya kifungo cha miaka minne jela binti wa miaka 19 baada ya kupatikana na hatia ya kumuua bila kukusudia mwanafunzi wa Chuo Kikuu cha Sayansi na Teknolojia Mbeya (MUST) baada ya kumchoma kwa kutumia kisu.

Hukumu hiyo ilitolewa mwishoni mwa wiki na Hakimu Mkazi Mwandamizi, Paulo Ntumo, mshtakiwa Suzan Castejeta (19), mkazi wa Ikuti Iyunga, ambaye alikuwa akituhumiwa kumuua Lunus Magesa mnamo Julai 17, 2020 katika eneo la Ikuti, Kata ya Iyunga jijini Mbeya.

Marehemu ambaye alikuwa mwanafunzi wa MUST, na mshtakiwa walikuwa na uhusiano wa kimapenzi na siku ya tukio wawili hao walikuwa na ugomvi.

Ugomvi huo ulikuwa ukielezwa na Jamhuri kuwa ndio uliomfanya mshtakiwa kumchoma kifuani mpenzi wake kwa kutumia kitu chenye ncha kali hali iliyosababisha kuvuja damu nyingi baada ya uchunguzi walibaini silaha iliyotumika ni kisu ambacho pia kilikutwa ndani ya chumba cha mshtakiwa huku kikiwa na damu.

Kwa mujibu wa wataalamu wa afya kupitia daktari, William Mulla, aliyefanya uchunguzi wa mwili wa marehemu alisema uvujaji damu ndio ulisababisha kifo chake muda mfupi wakati akiendelea kupatiwa matibabu katika Hospitali ya Rufani ya Kanda Mbeya.

Ilielezwa mahakamani hapo kuwa mstakiwa alipofikishwa mahakamani kwa mara ya kwanza mwaka jana alikana kutenda kosa hilo ndipo shauri hilo likapangwa kwa ajili kusikiliza siku nyingine na mshtakiwa alikiri kutenda kosa la kuua bila kudhamiria.

Baada ya kukiri kutenda kosa hilo kupitia mwanasheria wake wakili Irene Mwakyusa, Hakimu Ntumo kwa mamlaka aliyopewa na Mahakama Kuu ya Tanzania Kanda ya Mbeya, alimhukumu mshtakiwa Castejeta kwenda gerezani kutumikia kifungo cha miaka minne ili iwe fundisho kwake na kwa watu wengine hasa wanaoendekeza hasira na kuchukua uamuzi usiyo na busara na kudhuru au kuondoa uhai wa wenzao.

Alisema vitendo hivyo havina budi kukomeshwa katika jamii badala yake kunapotokea tofauti basi zitatufutiwe ufumbuzi kwa njia za halali bila kuathiri wengine wala kuvunja sheria za nchi.





## SMZ kuunganisha wadau kuzuia athari watu kuzama

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SERIKALI ya Mapinduzi ya Zanzibar (SMZ), imesema itahakikisha inawaunganisha wadau kutoka taasisi binafsi kwa ajili ya kutafuta mbinu za kuzuia athari za kuzama maji kwa watu visiwani Zanzibar hususan wanaotegemea kuendesha maisha yao kupitia fursa ya sekta ya uchumi wa bluu.

Akisoma hotuba kwa niaba ya Makamu wa Pili wa Rais wa Zanzibar, Hemed Suleiman Abdallah, Waziri Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu wa Baraza la Wawakilishi, Dk. Khalid Mohamed Salum, wakati wa kilele cha maadhimisho ya Siku ya Kuzuia Kuzama Duniani alisema hatua hiyo itasaidia watu ambao wanategemea fursa ya sekta hiyo kushiriki katika kazi zao za kiuchumi bila ya kuwa na hofu ya kupoteza uhai wao kwa kuzama na maji.

"Lengo la shughuli hii kwa hapa Zanzibar ni kulitangaza azimio la Umoja wa Mataifa juu ya kuchukua hatua za kuzuia kuzama na kutoa taarifa kwa jamii namna ya kuchukua tahadhari na kupunguza athari zinazotokana na kuzama ili kujenga uchumi kupitia sekta ya uchumi wa bluu," alisema.

alisema miezi iliyopita Umoja wa Mataifa ulipitisha azimio la kuzuia kuzama duniani na hiyo inatokana na kuongezeka kwa takwimu za matukio ya kuzama kwa watu hasa nchi za uchumi wa chini na wa kati.

"Zanzibar ikiwa ni miongoni mwa nchi hizo serikali itaendelea kuliangalia suala hilo kwa karibu zaidi na kulitafutia ufumbuzi wa kudumu ili kulipunguza na hatimaye kuliondoa kabia tatizo hili katika visiwa vyetu," alisema Makamu wa Pili wa Rais.

Alisema katika kuhakikisha Zanzibar inafikia azma ya maazimio hayo ya Umoja wa Mataifa, Taasisi ya Panje imeshirikiana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali Zanzibar kwa kutoa mafunzo ya kuwafundisha walimu 88 kuogelea kwa shule za Unguja na Pemba.

"Bila ya shaka hiyo itakuwa ni moja ya njia ya kuzuia na kupunguza athari ikiwa kutatokea hitilafu katika vyombo vyetu vya usafiri baharini pia itatoa fursa kwa vijana wetu kushiriki kwenye michezo ya kuogelea ndani ya nje ya nchi," alisema.

Alisema amefarijika kusikia kuwa Umoja wa Mataifa, Shirika la Afya Duniani (WHO), Taasisi ya Milele Foundation Zanzibar na Taasisi ya Panje, kuwawezesha wavuvi na wakulima wa mwani kupata ujuzi wa kuogelea na kufanya kazi zao za kila siku kwenye mazingira salama.

"Hatua hii ni kubwa sana na ni nzuri na itatupa 'credit' kwa jumuiya ya kimataifa kuwa tumeanza kupiga hatua katika kufanyia kazi mapendekezo ya azimio la Umoja wa Mataifa la kuzuia kuzama kote duniani," alisema.Kwa upande wake Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti kutoka Wizara ya Uchumi wa Bluu na Uvuvi, Sheha Idrisa Hamdani, alisema Zanzibar ikiwa ni sehemu ya kisiwa, serikali itahakikisha inatekeleza maazimio yaliowekwa na Umoja wa Mataifa ya kuzuia kuzama majini kwa watu.

# EU kuisaidia Zanzibar chanjo ya corona

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

JUMUIYA ya Ulaya (EU) imesema ipo tayari kuisaidia Zanzibar kupata chanjo ya corona kupitia mradi wa chanjo unaotolewa na jumuiya hiyo (COVAS) kwa ajili ya sekta mbalimbali ikiwamo utalii.

Hayo yalisemwa jana na Balozi wa Jumuiya ya Ulaya aliyepo Tanzania, Manfredo Fanti, wakati alipofanya mazungumzo na Waziri wa Afya, Ustawi wa Jamii, Jinsia na Watoto, Nassor Ahmed Mazrui, mjini Unguja.

Alisema jumuiya hiyo inatekeleza mradi wa chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona kupitia mradi wa COVAX ambao umelenga pia kuzisaidia baadhi ya nchi za bara la Afrika.

Alisema kupitia mradi wa COVAX wapo tayari kusaidia chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona kwa asilimia 20 sambamba na kuwataka wamiliki wa hoteli za kitalii waliopo Zanzibar kusaidia masuala ya chanjo kwa wafanyakazi wa sekta ya utalii.

"Jumuiya ya Ulaya ipo tayari kusaidia upatikanaji wa chanjo ya Covid-19 kupitia mradi wa COVAX na kuona wananchi wa Zanzibar wanapata chanjo ambayo itasaidia na kuwawezesha kuwa salama zaidi," alisema.

Naye Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui, alisema Zanzibar ipo tayari kupokea chanjo kwa ajili ya kujikinga na ugonjwa wa Covid -19, ili wananchi wanaotoa huduma mbalimbali katika sekta ya utalii wanakuwa salama.

Alisema katika hatua ya awali Zanzibar imepokea chanjo kwa ajili ya ugonjwa wa SINOVAC kutoka China huku akisisitiza milango ipo wazi kwa watu wengine kusaidia upatikanaji wa chanjo hizo.

Mazrui alisema chanjo iliyotolewa tayari imeanza kutumika kwa makundi mbalimbali ikiwamo wafanyakazi katika sekta ya afya ambao watakuwa wakihudumia wananchi na wagonjwa.

Aliyataja makundi mengine ambayo yatafaidika na chanjo ya kujikinga na ugonjwa wa corona ni wafanyakazi wanaotoa huduma katika Uwanja wa Ndege wa Abeid Amani Karume.

Makundi mengine ambayo yatafaidika na chanjo hiyo ni pamoja na watu wenye umri kuanzia miaka 40 hadi kuendelea ambao wapo katika hatari ya kushambuliwa na maradhi hayo kwa haraka.



Katibu wa Bunge, Nenelwa Mwihambi, akifungua kikao cha Baraza la Wafanyakazi wa Ofisi ya Bunge kinachofanyika kwa muda wa siku mbili katika Ofisi Ndogo ya Bunge Zanzibar, kushoto ni Katibu wa Baraza, Felister Njovu. **PICHA: BUNGE**

## Kadhi Mkuu awataka maimamu kudumisha amani

**Na Mwandishi Wetu,** ZANZIBAR

KADHI Mkuu wa Zanzibar, Shekhe Saleh Omar Kabi, amewataka maimamu na walimu wa madrasa za Kur-ani kutoa taaluma ya imani ya dini ya Kiislamu katika misikiti na madrasa ili kudumisha amani nchini.

Hayo yalielezwa katika ukumbi wa Msikiti wa Jaamiu Zinjibar Mazizini nje ya Mji wa Zanzibar wakati akizungumza na viongozi wa dini wakiwamo maimamu, na walimu wa madrasa pamoja na masheha wa shehia za Wilaya ya Magharibi 'A' na 'B' Unguja.

Alisema imani ya dini ya kiislamu imetoweka, hivyo iko haja ya walimu wa madrasa na maimamu kutoa taaluma kupitia misikiti na madrasa ili kurejesha hadhi, maadili, huruma, heshima na imani ya kweli ndani ya nyoyo za Wazanzibari.

Alisema udugu, upendo na ushirikiano wa pamoja utasaidia kuendeleza mbele dini ya kiislamu, na huepusha migogoro na kujenga amani na utulivu wa nchi.

Alisema, si vyema kujitokeza baadhi ya watu wachache kutaka kuuvuruga uislamu kwa kuleta migogoro ndani ya jamii jambo ambalo litasababisha mgawanyiko kwa waumini.

Naye Katibu wa Mufti wa Zanzibar Shekhe Khalid Ali Mfaume, alisema Ofisi ya Mufti hairidhishwi na vitendo mbalimbali vinavyofanya na baadhi ya Waislamu kwa kufanya udhalilishaji, malumbano ya mashehe katika mitandao ya kijamii pamoja na baadhi ya misikiti kushindwa kumwombea dua kiongozi mkuu wa nchi, baada sala ya Ijumaa.

"Waislamu wenzangu haipendezi kutomwombea dua kiongozi wetu wa nchi Rais wetu, Dk. Hussein Ali Mwinyi, Ijumaa jambo ambalo litasaidia mashirikiano ya pamoja katika kuijenga nchi yetu kwa amani na utulivu," alisema.

Alisema kutokana na vitendo visivyoridhisha katika baadhi ya madrasa, Ofisi ya Mufti imefanya uhakiki wa mashekhe, imegundua kuna baadhi ya mashekhe wameweka mbele msimamo yao sio dini na ndio inayoharibu uislamu.

"Wanatoa fatwaa wanaichukua kazi ya Mufti wakati kiongozi yupo anayetuongoza, mji mmoja hakuna nidhamu kila mtu anafuata ya kwake haipendezi hata kidogo," alisema Shekhe Khalid.

Naye Katibu Mkuu kutoka Jumuiya ya Friend of Zanzibar, Abubakar Kabogi, alisema dhana nzima ni kuhubiri amani utulivu na maendeleo ya waislamu hitilafu sio dhambi bali huzaa migogoro.

Alisema kuwa nafasi ya Zanzibar ni kubwa mno duniani, kwa jinsi inavyotatua migogoro katika nchi yake wenyewe, jambo ambalo nchi nyingine hushindwa kufanya hivyo.

Alisema kuwa kuwatii viongozi kutasaidia kujenga amani, upendo, mshikamano, maridhiano na utulivu wa Zanzibar.

Wakati viongozi hao wadini wakitoa taarifa hiyo, hivi karibuni mzee wa miaka 70 Muhammed Hamad, anadaiwa kumlawiti mtoto wa miaka 11 katika msikiti huko Masingini Wilaya ya Magharib 'A' Unguja na mtuhumiwa huyo yupo mikononi mwa Jeshi la Polisi Zanzibar.

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

### KUPOTEA KWA KADI YA GARI

**EXAVERY VICENT MWAULAMBO** ANATANGAZA KUPOTEA KWA KADI YAKE YA GARI YENYE NAMBA ZA USAJILI **T 513 DMP** - TOYOTA HARRIER. CHASSIS NAMBA **ACU150006522.** ENGINE NAMBA **Z872JG.** YEYOTE ATAKAYEIONA ATOE TAARIFA KITUO CHA POLISI. TAARIFA YA POLISI: **DAR/MAG/RB/367763/2021.**

116373102

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA**

**KATIKA MAHAKAMA YA MWANZO ENABOISHU WILAYA YA ARUMERU**

**SHAURI LA JINAI/MADAI NA. 75 YA 2021**

**FRANCISCO JAILOS KAOMBWE......MDAI/MLALAMIKAJI**

**Dhidi ya**

**ARAFA MOHAMED MUYA..........MDAIWA/MSHTAKIWA**

**HATI YA KUITWA SHAURINI (SUMMONS GENERAL)**
**(MCA. Na. 2/1984)**

**Kwa ARAFA MOHAMED MUYA WA NGULUBOBO**
Kwa kuwa umelazimika uhudhurie mahakamani ili ujibu shtaka/madai kuwa shahidi kama ifuatavyo
**FIKA MAHAKAMANI KUJIBU MADAI YA TSHS. 5,000,000/=**
**UNAAMRIWA NA JAMHURI** uhudhurie mbele ya mahakama hii siku ya Alhamisi tarehe 5.8.2021 saa 3:00 asubuhi au mara baada ya hapo ili shauri hili liweze kusikilizwa. USIKOSE KUHUDHURIA. Fahamu ya kwamba ukikataa kupokea hati hii na kuweka sahihi yako au ukipokea na kuacha kuhudhuria mahakamani ni kosa K/f Na. 114 A Sura ya 16 K/A. Hivyo Mahakama inaweza kukuchukulia hatua kali za kisheria.
**HATI HII IMETOLEWA NA AMRI YANGU NA MUHURI WA MAHAKAMA HII LEO TAREHE 22.7.2021.**

22-7-2021

116373002

---

**IN THE DISTRICT COURT OF DODOMA**
**AT DODOMA**

**PROBATE AND ADMINISTRATION CAUSE NO.49 OF 2021**

**In the matter of the Estate of the LATE LILIAN ANDREW SWAI of Kisasa within Dodoma city.**
**And**
**In the matter of Application for letters of Administration by NEEMA SAMMY SHUNDI**

**GENERAL CITATION**
**(RULE 75 OF PROBATE RULES GN 369 OF 1963)**

ALL PERSONS claiming to have any interest in the Estate of the above named deceased are hereby cited to come and see the proceedings if they think fit before the grant of letters of Administration is made to the above named Petitioner.
Objections to the grant should be filed on or before the 31 Day of 08 2021.
Dated at Dodoma this 23 day of JULY 2021.

RESIDENT MAGISTRATE
RESIDENT MAGISTRATE
DODOMA DISTRICT

116373402

---

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA TANZANIA**

**Katika Mahakama ya Mwanzo ya Wilaya ya Njombe**
**Kituo cha Njombe Mjini**
**Mkoa Njombe**

**Usimamizi wa Mirathi Na. 63/2021**

**Katika Shauri la Mirathi ya**
**BENALD LUPYANA MGINA..........MAREHEMU**
**Wa MELINZE**

**Katika Shauri la maombi ya kumteua Msimamzi yaliyotolewa na PAULINA SAMWEL MBAHA.....MWOMBAJI**

**TANGAZO KWA UMMA**
**(Kanuni ya 5(2) ya Kanuni za Usimamizi wa mirathi Mahakama za Mwanzo)**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote/maslahi yoyote na mirathi ya marehemu tajwa hapo juu, wanaalikwa kuja na kuhudhuria katika shauri hili endapo wakitaka kufanya hivyo mnamo tarehe 24 Mwezi 08 Mwaka 2021 kabla huyo mwombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo. Mapingamizi yoyote kuhusu maombi haya yawe yameandikishwa kabla au mpaka tarehe tajwa hapo juu.
Zingatia; Endapo kuna yeyote mwenye wosia wa Marehemu anaweza kuuleta Mahakamani kukaguliwa.
Wosia wa Marehemu huyo upo Mahakamani na waweze kukaguliwa
Imetolewa leo tarehe 22 Mwezi 07 Mwaka 2021.

116373502

---

### KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**SULEIMAN HASSANI RWAIKONDO**
Anatangaza kupotelewa na Kadi ya Gari aina ya **TOYOTA SIENTA**
yenye namba ya usajili **T 611 DDV**
Yenye rangi nyeusi
Chassis namba **NCP10040178**
Engine namba **INZEAA0178**
Yeyote atakayeiona atoe taarifa Kituo cha Polisi.
Taarifa ya Polisi: **GEI/CHA/RB/357529/2021.**

116373302

---

### KUPOTEA KWA CHETI



**DOREEN ALFRED** anatangaza kupotelewa na cheti cha kidato cha nne chenye index namba **P 0321-0060,** kilichotolewa na baraza la mitihani kupitia shule ya secondary KINONDONI mwaka 1995,yeyote atakayekiokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **KW/RB/3667/2021**

116373702

---

**JAMUHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA)**
**YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika Mahakama ya Mwanzo MJINI MOROGORO**
**Usimamizi wa Mirathi**
**NO.216/2021**

Ombi la **PETER ATANAS ANDREA** Kuteuliwa Msimamizi wa Mirathi ya Marehemu **ATANAS ANDREA LUBISI**
Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaalikwa kuja kuhudhuria shaurini mnamo **tarehe 18/08/2021** kabla huyo mwambaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.
Wosia wa marehemu huyo upo hapa mahakamani waweza kukaguliwa.
**Tarehe 15/07/2021**

116374202

---

## OFISI ZA MATANGAZO MIKOCHENI INDUSTIAL AREA, PO.BOX 31042, DAR ES SALAAM. MOB: +255 - 0782253676

**Kwa Habari Motomoto**

usikose Gazeti lako

la Nipashe kila siku

Tupigie

0782253676

Nipashe MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

HABARI KIMATAIFA

# Waganda wahoji kila mbunge kupewa mil. 200/- anunue gari

**Kampala,** UGANDA

WABUNGE 529 wa Bunge la Uganda wiki hii kila mmoja, amepokea Sh. milioni 200 za Uganda, kwa ajili ya kununua magari ya viongozi waliochaguliwa.

Taarifa hiyo imepokelewa shingo upande na raia wa Uganda, kutokana na nchi kuathirika vibaya na mgogoro kiafya unaosababishwa na janga la Covid-19.

Msemaji wa Serikali Ofwono Opondo, ametetea uamuzi huo, akisisitiza kwamba wabunge wana haki ya kusafiri kwa kutumia kipando, akitoa mfano wa mila ya zamani.

Uamuzi haukupokelewa vema na wananchi wote. Sarah Bireete, mwanaharakati wa haki za binadamu, anashutumu hatua hiyo iliyochukuliwa katikati ya Covid-19 lililoathiri nchi na kusambaa maeneo mbalimbali ya nchi.

"Kipaumbele kinapaswa kuwa chanjo kwa raia, kufanya vipimo, ili kujua walioambukizwa virusi hivyo na kuhudumia wagonjwa wa Covid-19. Tunapoona uamuzi uliochukuliwa na serikali kununulia magari wabunge, wakati hatuna pesa za kutosha kwa chanjo na hospitali hazina dawa muhimu na oksijeni, vipaumbele vya nchi vimebadilishwa. Watu wasiojali maisha ya watu, maslahi yao," alisema mwanaharakati huyo.

"Mawaziri tayari wana magari mawili kila mmoja na dereva na huku wakipewa mafuta kwa matumizi ya magari hayo ambayo yanalipwa na wananchi kupitia kodi wanazotozwa. Unaona kuwa wananchi ndio wanaendelea kumizwa."

Hasira ziliibuka katika vyombo vya habari na kwenye mitandao ya kijamii.

Mnamo mwaka 2018, hatua kama hiyo pia ilisababisha mvutano na waandamanaji walivamia makao makuu ya Bunge.

Joseph Ochieno, mwanasiasa na mchanganuzi wa siasa za Uganda, alisema maandamano haya hayatabadilisha chochote.

**RFI**



Wavuvi wakivua samaki kwenye Mto Nile, uliokatisha kwenye daraja mjini Khartoum, nchini Sudan, mwishoni mwa wiki. **PICHA: XINHUA**

## Mtuhumiwa jaribio mauaji Rais Goïta afariki kizuizini

**Bamako,** MALI

MTU anayetuhumiwa kujaribu kumuua rais wa mpito Mali Kanali Assimi Goïta, kwenye Msikiti Mkuu wa Bamako wiki iliyopita, amefariki dunia akiwa chini ya ulinzi wa polisi, Julai 25, serikali ya Mali imetangaza.

Chanzo cha usalama Mali, kiliwaambia waandishi wa habari, afya ya mshambuliaji wa rais wa mpito imedhoofika, yuko hospitalini.

Waziri Mkuu wa Mali Choguel Maïga, alikutana na rais wa mpito, Kanali Assimi Goïta na muda mfupi baadaye kifo cha mtuhumiwa huyo kilitangazwa.

Sababu ya kifo chake haijaelezwa ingawa maiti inafanyiwa uchunguzi kupitia vipimo vya damu kubaini sababu ya kifo chake.

Mwanamume huyo anatuhumiwa kujaribu kumdunga kisu rais wa mpito Goïta, wiki iliyopita wakati alipohudhuria sala katika msikiti.

Mamlaka Mali inaamini kwamba kuna watu wengine wanaohusika katika jaribio la kumuua mkuu wa nchi.

**RFI/BBC**

## Ufaransa yaridhia muswada chanjo corona kuwa lazima

**Paris,** UFARANSA

BUNGE la Ufaransa limeridhia muswada ambao utafanya chanjo ya Covid-19 kuwa ya lazima kwa wafanyakazi katika sekta ya afya pamoja na matakwa kuviongezea nguvu vithibitisho vya afya kwa maeneo ya kijamii ya wazi.

Hatua hiyo inaridhiwa wakati Ufaransa ikikabiliana na wimbi la nne la maambukizi ya virusi vya corona na kukabili wimbi la nne la corona.

Wanaohudhuria katika majumba ya makumbusho, sinema au mabwawa ya kuogelea wanazuiwa kuingia katika maeneo hayo, kama hawataonyesha vithibitisho vya kupata chanjo ya Covid-19 au kufanya vipimo vya karibuni dhidi ya virusi vya corona.

Ufaransa ipo katika makabiliano ya corona katika kirusi aina ya Delta ambacho kinaambukiza kwa kasi.

**DW**

## Huawei yawekeza Dola Mil. 150 kwa vipaji

**Shenzhen,** CHINA

HUAWEI inatarajia kuwekeza dola za kimarekani milioni 150 katika kukuza vipaji vya dijitali, kipindi cha miaka mitano ijayo, mpango ambao utafaidisha vijana wengine milioni tatu.

Makamu Rais wa Huawei Kanda ya Kusini mwa Afrika Yang Chen, alisema Huawei imejitolea kwa maendeleo ya rasilimali kwa watu Afrika.

Aidha, Mwenyekiti wa Huawei Liang Hua alisema dola milioni 150 katika mpango huo kwa kipindi cha miaka mitano ijayo, zitasaidia wanafunzi wa vyuo vikuu na vijana kuboresha ujuzi wao wa dijitali.

"Afrika ina idadi kubwa ya vijana, hawa ndio rasilimali kubwa ya bara hili, itaimarisha uchumi katika siku zijazo. Huawei inashirikiana na serikali za Kiafrika, taasisi za elimu na tasnia, ili kuwapa viongozi wa siku zijazo maarifa ya kisasa katika kiwango cha juu duniani, kuwapa fursa ya kutumia maarifa kuleta maendeleo barani.

"Leo tunatangaza mwendelezo wa mpango wa mbegu za kizazi kijacho cha Huawei 'Huawei's Seeds for the Future Program 2.0' kama sehemu ya ahadi yetu ya kuendelea kukuza vipaji," alisema Hua.

Mwaka 2008, Huawei ilianza kupanua programu zake za kukuza vipaji kupitia ufadhili wa masomo, mashindano ya teknolojia na mafunzo ya ustadi wa dijitali na kunufaisha zaidi ya watu milioni 1.54 kutoka nchi zaidi ya 150.

Kutoka kwa Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia, Katibu Mkuu, Dk. Leonard Akwilapo, alisifia mpango wa huo na kwamba ni muhimu wake katika kuwezesha ujuzi wa kuajiriwa.

"Mpango huu unadumisha ushirikiano kati ya Wizara ya Elimu, Sayansi na Teknolojia na Huawei Tanzania katika kukuza mahusiano endelevu ya rasilimali watu katika ICT."

## Rais Nyusi auona ushindi dhidi ya waasi

**Cabo Delgado,** MSUMBIJI

RAIS wa Msumbiji, Filipe Nyusi, amesema wanajeshi wanaopambana na waasi wenye uhusiano na kundi la Islamic State (IS) katika mkoa wa Kaskazini wa Cabo Delgado, wanaendelea kupata ushindi uwanjani na adui amerudi nyuma.

Nyusi alikuwa akilihutubia taifa juzi kuhusu mzozo uliopamba moto wakati waasi wakishambulia mji wa pwani wa Palma, Machi, karibu na miradi ya gesi yenye thamani ya dola bilioni 60 ambayo ilikuwa inalenga kubadilisha uchumi wa Msumbiji.

Akitoa hotuba hiyo kupitia televisheni na mitandao ya kijamii, Nyusi alitangaza wanajeshi wa Jumuiya ya Maendeleo ya Nchi za Kusini mwa Afrika (SADC), wanahamasishwa kuingilia kijeshi mkoa wa Cabo Delgado, ulioko chini ya uasi wa kijihadi.

Ombi la SADC kuingilia kati mzozo wa Cabo Delgado, limekamilishwa rasmi, Waziri wa Ulinzi Msumbiji Jaime Neto, ameliambia shirika la habari la AFP, kwa njia ya simu.

**VOA**

HABARI MICHEZO

# RONALDO haondoki Juventus - Nedved




**TURIN, Italia**

CRISTIANO Ronaldo atabakia Juventus licha ya uvumi kwamba, ataondoka kabla ya kuanza kwa msimu mpya, kwa mujibu wa makamu rais wa klabu hiyo ya Ligi Kuu ya Italia, Serie A, Pavel Nedved.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Ureno amebakiza mwaka mmoja kwenye mkataba wake wa miaka minne aliousaini wakati alipohamia hapo akitokea Real Madrid kwa dau la euro milioni 112.

Ronaldo amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka hapo Turin kabla ya kuanza kwa msimu mpya, huku klabu zake za zamani, Manchester United na Real Madrid zikiwa ni miongoni mwa sinazomwania pamoja na Paris Saint-Germain.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 36 alifunga mabao 29 kwa msimu wa 2020-21 na kuwa mfungaji bora wa Ligi, tuzo ambayo amewahi pia kushinda kwenye Ligi Kuu ya England na ile ya Hispania, LaLiga.

"Ronaldo amerudi mazoezi na klabu na atabakia na sisi," alisema Nedved akiiambia Sky Sport Italia.

Nedved alizungumzia majaliwa ya Ronaldo baada ya Juve kuifunga Cesena 3-1 kwenye mchezo wa kirafiki wa maandalizi ya msimu mpya Jumamosi, na aliulizwa pia kuhusu majaliwa ya Paulo Dybala na Giorgio Chiellini.

Fowadi wa Argentina, Dybala mwenye umri wa miaka 27, pia anaingia kwenye mwaka wake wa mwisho katika mkataba wake na klabu yake hiyo ya Serie A na Nedved alibainisha kuwa wanatarajia kuanza mazungumzo nae kuhusu mkataba mpya.

## WIJNALDUM ATOBOA SIRI KUONDOKA LIVERPOOL



**PARIS, Ufaransa**

GEORGINIO Wijnaldum amefunguka kuhusu sababu ya yeye kuondoka Liverpool kipindi hiki cha majira ya joto na kusema alihisi "kupendwa na kuheshimiwa" na klabu nyingine.

Wijnaldum mwenye umri wa miaka 30, alijiunga na Paris Saint-Germain kwa uhamisho huru baada ya mkataba wake kumalizika kule Anfield baada ya kukaa miaka mitano na miamba hao wa Ligi Kuu England.

Kiungo huyo alikuwa nguzo muhimu kwa Liverpool wakati wakishinda kombe la Ligi ya Mabingwa Ulaya mwaka 2019 pamoja na taji la kwanza la Ligi Kuu ya England kwa kipindi cha miaka 30, lakini amesema alihisi kutothaminiwa.

"Kuna wakati nilihisi kutopendwa wala kuthaminiwa," alisema akiwaambia waandishi wa habari.

"Sio wachezaji wenzangu, sio watu wa pale kwneye kambi ya mazoezi Melwood.

"Kutoka kwako nilijua, naweza kusema wote walinipenda na mimi niliwapenda. Lakini walikuwa baadhi ya watu ambao hawakunipenda wala kunithamini."

Wijnaldum alipewa heshima ya wachezaji kusimama wakati wa mchezo wake wa mwisho Liverpool baada ya kushinda 2-0 dhidi ya Crystal Palace na kufanikiwa kumaliza kwenye nne bora msimu uliopita.

## Ancelotti amtaka Dalot Real Madrid



**MADRID, Hispania**

KOCHA wa Real Madrid, Carlo Ancelotti ameonyesha nia ya kutaka kumsajili beki wa kulia wa Manchester United, Diogo Dalot na amemtaja kuwa ni lengo lake muhimu.

Dalot mwenye umri wa miaka 22 aliwasili hapo Old Trafford mwaka 2018 kwa pauni milioni 19 na hajang'ara na haionyeshi kama atapewa nafasi mwaka huu wakati Aaron Wan-Bissaka akiwa mbele yake kupata namba kikosi cha kwanza, huku United pia ikimfuatilia Kieran Trippier wa Athletico Madrid.

Inavyoonekana Dalot, ambaye alitumikia kwa mkopo AC Milan msimu uliopita, anaweza kukumbwa na hali hiyo msimu huu pia huku ripoti kadhaa huko Hispania zikidai Ancelotti ana nia kumsajili beki huyo.

Na sasa Ancelotti ameonyesha nia ya kutaka huduma ya mlinzi huyo kwa ajili ya kuimarisha kikosi chake tayari kwa kuanza msimu mpya wa Ligi Kuu.


Kwa mujibu wa Marca, Ancelotti ameuambia uongozi wa klabu hiyo wamsajili Dalot kwani anaweza kuwa msaada mkubwa kwa kikosi hicho kwenye safu ya ulinzi.

Ikumbukwe kuwa Real Madrid imeachana na beki wake mkongwe Sergio Ramos ambaye ametimkia PSG akiwa mchezaji huru.

# HABARI MICHEZO

## ARSENAL YATENGA DAU KWA LOCATELLI

**LONDON, England**



KLABU ya Arsenal imewasilisha ombi la pauni milioni 34 kumsajili kiungo Manuel Locatelli wa Sassuolo ya Italia, wakala wa nyota huyo amethibitisha.

Washikabunduki hao wamekuwa wakihusishwa kumsajili nyota huyo wa Italia mwenye umri wa miaka 23 wakati Mikel Arteta akitaka kuimarisha sehemu ya kiungo ya klabu hiyo kabla ya msimu wa 2021-22 kuanza.

Tayari Arsenal imemsajili Albert Sambi Lokonga wiki hii kwa dili la pauni milioni 18 kutoka Anderlecht.

Klabu hiyo ya Kaskazini ya London itakutana na ushindani mkali wa kugombea saini ya Locatelli kutokana na kibibi cha Turin, Juventus.

Klabu hiyo ya Italia imekuwa katika harakati za kuitaka saini ya nyota huyo wa timu ya taifa ya Italia, ambaye aling'ara kwenye michuano ya Euro 2020.

Arsenal ilikuwa timu ya kwanza kuonyesha ni ya kuwania saini ya nyota huyo, lakini Juventus nao wamekuwa wakimwania kwa udi na uvumba.



## BARCELONA KUTEMA MABEKI WATATU

**BARCELONA, Hispania**

BARCELONA imeripotiwa kuwa itawaruhusu mabeki, Clement Lenglet, Sergino Dest na Samuel Umtiti kuondoka klabuni hapo mapema wiki hii iwapo ada za kutosha zitapatikana.

Klabu hiyo ya Katalunya imejikuta kwenye matatizo ya kifedha hivyo kuilazimu kuuza wachezaji kwa haraka, ili kupunguza bili ya mishahara.

Kwa mujibu wa mtandao wa soka wa Sport wa Hispania mabeki Lenglet, Dest na Umtiti wanaweza kuondoka siku chache badala ya wiki kadhaa zijazo iwapo maombi yanayofaa yatawekwa mezani.

Ripoti zimedai wapinzani katika Ligi Kuu ya England Arsenal na Tottenham zina nia kumsajili Lenglet huku mabingwa wa Ujerumani, Bayern Munich na bingwa wa Serie A, Inter Milan zinamfuatilia Dest.

Umtiti amehusishwa na mpango wa kurejea Lyon alikokuwa kabla ya kujiunga na Barcelona miaka mitano iliyopita.

Barcelona inahitaji kwa kiasi kikubwa kuboresha hali yao ya kifedha baada ya kuwa na deni la zaidi ya pauni bilioni moja.

## MAN CITY KUMKOSA LEWANDOWSKI

**MANCHESTER, England**

MANCHESTER City wanaripotiwa kuwa "hawana nafasi" ya kumpata Robert Lewandowski wa Bayern Munich msimu huu wa majira ya joto.

Mkataba wa mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 32 kule dimba la Allianz Arena unamalizika mwishoni mwa msimu wa 2022-23, na awali alikuwa amekataa kukanusha uhamisho kwenda ligi nyingine.

Man City wanatarajiwa kumuweka Harry Kane kama kipaumbele kwa msimu huu wa joto, lakini ikiwa watapewa bei kubwa ya uhamisho wa nahodha huyo wa England, wataelekeza nguvu kwa Lewandowski.

Hata hivyo, chanzo kutoka Ujerumani kinadai kuwa hakuna "nafasi" ya Lewandowski kuondoka Bayern katika wiki zijazo, licha ya hali yake ya mkataba kutokuwa na uhakika.

Bayern inadaiwa wanaamini kwamba wakala wa Lewandowski, Pini Zahavi anafanya ujanja ujanja katika jitihada za kuongeza mshahara wa mshambuliaji huyo na kocha Julian Nagelsmann amekiri kuchanganywa na dhana ya kinachoendelea juu ya nyota wake.

Lewandowski alifunga mabao 41 katika michezo 29 ya Ligi Kuu ya Ujerumani, Bundesliga, muhula uliopita, akivunja rekodi ya awali ya wakati wote ya mabao 40 iliyowekwa na Gerd Muller msimu wa 1971-72.



## KWA UFUPI

### VARANE AKARIBIA MAN
KLABU ya Manchester United inakaribia kufikia makubaliano na Real Madrid kwa ajili ya kumsajili mlinzi wa Ufaransa, Raphael Varane mwenye umri wa miaka 28, kwa dau la pauni milioni 42. ***(Marca)***

### NIGUEZ ATAKIWA
MANCHESTER United pia wanaweza kumsajili kiungo wa Hispania, Saul Niguez kutoka kwa mabingwa wa LaLiga Atletico Madrid kwa dau la pauni milioni 45. Nyota huyo mwenye umri wa miaka 26 anahusishwa pia na klabu za Barcelona na Juventus. ***(Mail)***

### MALEN AWANIWA DORTMUND
KLABU ya Borussia Dortmund inaonekana kukamilisha mpango wa kumsajili nyota anayewaniwa na Liverpool, Donyell Malen mwenye umri wa miaka 22 kwa dau la pauni milioni 26. ***(Fabrizio Romano)***

### LAMELA AKARIBIA SEVILLA
WINGA wa Argentina, Erik Lamela mwenye umri wa miaka 29, anakaribia kukamilisha uhamisho wake kutoka Tottenham Hotspur kwenda Sevilla, huku Winga wa Hispania, Bryan Gil mwenye miaka 20, akielekea upande wa pili. ***(Marca)***

### BARKLEY ATAKIWA NEWCASTLE
NEWCASTLE United watamgeukia kiungo wa Chelsea na England, Ross Barkley mwenye umri wa miaka 27, ikiwa watashindwa kumsajili, Joe Willock mwenye miaka 21, kutoka Arsenal. ***(The Athletic)***

### JUVE WAMKOMALIA LOCATELLI
JUVENTUS imepanga kufanya mazungumzo mengine mapya na Sassuolo wakipambana kumshawishi kiungo wa Italia, Manuel Locatelli anayewaniwa pia na klabu ya Arsenal. ***(Goal)***

### PSG YAMTAKA KOULIBALY
KLABU ya Paris St-Germain wamefanya mazungumzo na wakala wa Kalidou Koulibaly katika harakati zao za kumsajili mlinzi huyo wa Napoli na Senegal mwenye umri wa miaka 30 ***(Corriere dello Sport)***

### ISCO KUTOPEWA MKATABA
KIUNGO wa Hispania, Isco mwenye umri wa miaka 29 hatapewa mkataba mpya na klabu yake ya Real Madrid. Mkataba wake wa sasa unamalizika msimu ujao. ***(AS)***

### POBGA ATAKIWA KUBAKI
KOCHA wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer anataka kiungo wake, Paul Pogba mwenye umri wa miaka 28, kubakia katika klabu hiyo, huku Paris St-Germain ikimtaka . ***(Manchester Evening News)***

### CORREA AWINDWA
KLABU za Arsenal, Tottenham na Everton zinamwania Joaquin Correa mwenye umri wa miaka 26, ambaye anatarajiwa kuondoka Lazio msimu huu. ***(Corriere dello Sport)***

### CHIESA HAUZWI
JUVENTUS wamekataa dau la pauni milioni 86 kutoka kwa Liverpool kwa ajili ya kumuuza, Federico Chiesa mwenye umri wa miaka 23. ***(Republica)***

# DONDOO ZA SOKA
## MAGAZETI YA ULAYA




# INTER YAKATAA KUMUUZA LUKAKU

**Bosi wake asema ana uhakika ataendelea kucheza hapo kwani yupo kwenye mipango na...**

**MILAN, Italia**

OFISA Mtendaji Mkuu wa Inter Milan, Beppe Marotta, amesisitiza Romelu Lukaku hauzwi, wakati huu kukiwa na uvumi juu ya majaliwa ya nyota huyo wa kimataifa wa Ubelgiji.

Lukaku amekuwa akihusishwa na mpango wa kuondoka kwa mabingwa hao wa Italia baada ya kuondoka kwa kocha mkuu, Antonio Conte, huku Nerazzurri hao wakiwa kwenye matatizo ya kifedha yaliyosababishwa na mlipuko wa virusi vya corona.

Nyota huyo mwenye umri wa miaka 28 ameripotiwa kuwaniwa na klabu yake ya zamani ya Chelsea na mabingwa wa Ligi Kuu ya England, Manchester City.

Akizungumza kabla ya mchezo wa kirafiki kati ya Inter na Pergolettese, Marotta alisema Lukaku haondoki hapo kwenye dimba la San Siro.

"Kwa upande wetu, tunaweza kusema kwa uhakika kabisa Lukaku hauzwi," alisema Marotta akinukuliwa na Sportmediaset.

"Lukaku ni mchezaji muhimu na kocha wetu mkuu Simone Inzaghi ana mipango nae kwa msimu unaokuja."

Lukaku alifunga mabao 24 katika mechi 36 za ligi kwa msimu wa 2020-21, huku akitoa pasi za mabao 11.

Katika msimu wa 2016-17 akiwa anacheza kule Everton, Mbelgiji huyo alifunga mabao 25 kwa msimu mmoja.

Lukaku jana Jumatatu alitarajiwa kuanza mazoezi kwa mara ya kwanza chini ya kocha, Inzaghi.

HABARI MICHEZO

# SIMBA SASA INAWAZIA UBINGWA WA AFRIKA

**Na Saada Akida, KIGOMA**

BAADA ya kufanikiwa kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania kwa mara ya nne mfululizo na Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (FA) mara mbili mfululizo, uongozi wa Simba sasa wanataka kutawala soka la Afrika.

Akizungumza na gazeti hili mjini hapa, Makamu Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi wa Simba, Salim Abdallah 'Try Again' amesema sasa wanataka kutawala soka la Afrika, kwa kuchukua ubingwa ndani ya mwaka mmoja au miwili ijayo.

Alisema msimu huu malengo yao hayakutimia kwa sababu waliishia kwenye hatua ya robo fainali ya Ligi ya Mabingwa Afrika na wanajipanga vizuri kwa ajili ya kutawala soka la Afrika.

"Msimu umekwisha katika michuano ya kimataifa tumeishia robo hayakuwa malengo yetu, lakini tunatarajia baada ya mwaka mmoja au miwili ijayo Simba itatawala soka la Afrika kwa sababu tunakuja na mipango mizuri," alisema Try Again.

"Kuhusu ligi ya nyumbani tumefanikiwa kutwaa ubingwa mara nne na FA mara mbili mfululizo, bado hatujamaliza kwa sababu tunahitaji kuchukua makombe yote ya hapa nyumbani, siku chache zijazo tutaanza maandalizi ya Ngao ya Hisani," alisema.

Alisema malengo yao kuchukua makombe yote wanayoshiriki sasa wanajipanga kutwaa Ngao ya Hisani ili kutimiza malengo yao, ana wahakikishia mashabiki wa Simba kwamba wamejipanga vizuri.

"Tunakwenda vizuri tumetulia, tunapanga mipango yetu kwa namna tunavyofahamu, wanachama na mashabiki wasubiri waone shughuli inavyofanyika," aliongeza kusema.



Wasanii mbalimbali wa muziki kutoka Zanzibar, wakifuatilia kwa umakini semina maalumu juu ya namna bora ya kukuza vipaji vya muziki visiwani humo. Semina hiyo ni sehemu ya Tamasha la Zuchu Home Coming na Zantel litakalofanyika Agosti 21, katika Viwanja vya Amani Zanzibar. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Biashara United yaacha 14

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United ambayo msimu ujao itacheza michuano ya Kombe la Shirikisho la Soka Afrika (CAF), imetangaza kuwaacha wachezaji 14 ambao hawatokuwa nao tena na wako huru kujiunga na timu zingine.

Mtandao rasmi wa klabu hiyo umeandika kuwa umeachana na wachezaji hao na kuwatakia kila la kheri huko waendako.

"Wanajeshi wa mpakani, tunawashukuru kwa mchango wao waliotoa kwenye klabu yetu kipindi chote walichokuwa nasi na tunawatakia kila la kheri huko waendako." Iliandika klabu hiyo kwenye mtandao wake wa kijamii.

Wachezaji walioachwa na klabu hiyo ni Hassan Mkindili, Jonathan Zephania, Ally Mwasomola, Jackson Edward, Baraka Makoba na Angelo Malima.

Wengine ni Yusuph Abdulwaheed, Ambrosi Ayoy, Yusuph Jamali, Juma Mpakala, Mussa Balozi, Kauswa Manumbu, Tariq Simba, na Joseph Zziwa.

Kuachwa kwa wachezaji hao kunatoa fursa ya klabu hiyo kujipanga na kusajili wachezaji wengine kwa ajili ya Ligi Kuu msimu ujao, lakini kikubwa zaidi ni kupata wachezaji bora zaidi ambao watakaiwakilisha vyema kwenye michuano ya Kombe la Shirikisho.

Majuzi, Katibu Mkuu wa klabu hiyo, Haji Mtete, alisema kuwa watasajili wachezaji bora wa ndani na nje ya nchi, huku akisema kipaumbele kimewekwa zaidi kwenye nafasi ya ushambuliaji, baki wa kati na kiungo.

"Tunakwenda kucheza mechi za kimataifa. Tunakwenda kucheza michuano mikubwa na wachezaji wa viwango vya juu kwa hiyo na sisi lazima tujiimarishe. Lengo letu ni kwenda kwenye michuano hiyo tukiwa na wachezaji wenye viwango vikubwa na wazoefu," alisema.

## Zanzibar yajipanga michezo ya majeshi

**Na Hawa Abdallah, ZANZIBAR**

TIMU zinazoshiriki michuano ya Majeshi Kanda ya Zanzibar, zinatarajiwa kuondoka mapema Agosti Mosi kuelekea Dodoma kunakofanyika michuano hiyo.

Akizungumza na gazeti hili Katibu wa BAMATA Kanda ya SMZ, Sheha Mohmed, alisema kuwa tayari washafanya mchujo wa mwisho kwa upande wa timu za Kanda ya Zanzibar kwa wachezaji watakaosafiri katika michuano hiyo.

Alisema kwa Kanda ya SMZ inatarajia kushiriki michuano yote saba ikiwamo mpira wa miguu, kikapu wanawake na wanaume, pete kwa wanawake, wavu wanawake na wanaume, mpira wa mikono, mbio za riadha pamoja na kulenga shabaha.

Alisema timu zote saba zinaendelea na mazoezi ya mwisho katika viwanja walivyopangiwa ili kuhakikisha zinafanya vizuri katika michuano hiyo.

Kwa upande wa mpira wa miguu tayari wameshacheza mechi mbalimbali za kirafiki kwa madaraja tofauti na zile timu za mchanganyiko, ili kupata timu nzuri itakayoweza kushindana.

"Tunaendelea na mazoezi, ili kuona tunajiandaa vizuri katika kuhakikisha tutakwenda kushindana na tunarudi na ushindi, timu zetu zote zinaendelea na kucheza mechi za kirafiki ili kuhakikisha tunapata timu zenye viwango.

Michuano hiyo ya BAMATA inatarajiwa kuanza kutimua vumbi lake Agosti 4 hadi 13 huko Dodoma.

## Lwanga: Simba itafunika tena msimu ujao

**Na Saada Akida, KIGOMA**

KIUNGO mkabaji wa Simba, Taddeo Lwanga amekiangalia kikosi cha timu hiyo na kudai kwamba bado wataendelea kutesa kutokana na ubora walionao kwa msimu ujao.

Mfungaji huyo wa bao pekee lililoipa Simba ubingwa wa kombe la Shirikisho la Soka Tanzania (FA), Lwanga, alisema mafanikio yao msimu huu yametokana na ushirikiano wa wachezaji, benchi la ufundi, viongozi hadi mashabiki hali hiyo anatarajia kuwepo ndani ya klabu hiyo.

Raia huyo wa Uganda alisema Simba ni bora kuanzia kikosi hadi uongozi ikilinganishwa na watani wao Yanga, hivyo anaiona ikiendelea kutawala soka la Tanzania hadi Afrika kwa siku za usoni.

"Nikiangalia kikosi cha Simba naona kitaendelea kutawala soka la Tanzania kutokana na ushirikiano mzuri ndani ya klabu hii," alisema.

"Ni kweli tumechukuwa ubingwa kwa kuwafunga Yanga ikiwa pungufu na kushinda bao 1-0 kwamba wapinzani wao ni wagumu, haijalishi hilo kwa sababu Simba ni Bingwa wa ligi na hii FA, tena mfululizo," alisema Lwanga.

Michezo
Jumanne Julai 27, 2021
Nipashe



## Inter yakataa kumuuza Lukaku

HABARI UK. 22




Nahodha Msaidizi wa Mabingwa wa mashindano ya Kombe la FA, Mohammed Hussein 'Zimbwe Jr ', akionyesha kombe la michuano hiyo muda mfupi kabla ya kuingia kwenye ndege kurejea jijini Dar es Salaam jana asubuhi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SIMBA YAIPIGA YANGA KIJEMBE

## ●●●Ni baada ya kufanikiwa kutetea taji la Kombe la FA na Ligi Kuu Tanzania Bara mfululizo...

**Na Somoe Ng'itu, KIGOMA**

WACHEZAJI na mashabiki wa Simba wamewananga watani zao baada ya kufanikiwa kutetea ubingwa wa mashindano ya Kombe la FA kwa kutamba "vijana wanashinda mechi, wanaume wanashinda mataji."

Kauli hiyo ilitolewa na nyota mbalimbali wa Simba juzi baada ya timu yao kupata ushindi wa bao 1-0 katika fainali ya Kombe la FA iliyochezwa kwenye Uwanja wa Lake Tanganyika mkoani hapa ikiwajibu Yanga ambao waliibuka kidedea kwenye mchezo wa mzunguko wa pili wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Akizungumza na gazeti hili, kipa chaguo la kwanza, Aishi Manula alisema timu yao imeonyesha ubora na imetimiza vyema malengo waliokuwa wamejiwekea katika msimu wa 2020/21.

Manula alisema haikuwa kazi rahisi kumaliza msimu kwa kutetea makombe yote makubwa hapa nchini na vile vile kucheza hatua ya robo fainali ya michuano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika.

"Tunasema vijana wanashinda mechi, wanaume wanashinda makombe, asanteni sana wana Simba wote," alisema Manula huku akibusu medali yake.

Kiungo Mzamiru Yassin alisema wachezaji wakubwa wanashinda mataji na wachezaji wadogo wanashinda mechi.

"Tumemaliza kazi tuliyoifuata, hakika ulikuwa ni msimu wenye ushindani na heka heka za kila aina, tukutane tena msimu ujao," alisema kiungo huyo aliyejiunga na Simba akitokea Mtibwa Sugar.

Ofisa Mtendaji Mkuu wa Simba, Barbara Gonzalez, alisema kama angepata nafasi ya kuulizwa anahitaji kushinda mechi (dabi), au kombe yeye angechagua kombe na si kitu kingine.

"Naomba niseme sisi kama menejimenti ya Simba tumetimiza majukumu yetu, hiki tulichopata ndio ilikuwa malengo yetu, tumefanya jitihada zote kuhakikisha tunafikia malengo," alisema Barbara.

Alisema kila mmoja ndani ya klabu anatakiwa kupongezwa, mafanikio waliyopata ni makubwa na yamewawekea heshima ndani na nje ya Tanzania.

"Tumefanikiwa kuonyesha ukubwa wetu, uzito kwa kupata ushindi, na kama ungewahi kuniuliza kati ya ushindi wa mchezo mmoja na kombe, hakika ningekwambia ninahitaji kombe tu na si ushindi," alimaliza kiongozi huyo.

Naye nahodha wa Yanga, Bakari Mwamnyeto alisema walijitahidi kucheza katika kiwango cha juu lakini hawakufanikiwa kupata matokeo mazuri kama ilivyokuwa kwa wapinzani wao.

Mwamnyeto pia alisema walinipanga kucheza vyema ili kusaka ushindi lakini kadi nyekundu aliyoonyeshwa kiungo wao, Mukoko Tonombe iliwapunguzia nguvu.

"Kadi nyekundu ya Mukoko ilitugharimu, lakini hatujakata tamaa, tunaenda kujitathmini na kujipanga upya kwa ajili ya msimu mpya," alisema Mwamnyeto.

Naye Mjumbe wa Kamati ya Mabadiliko, Hersi Said, alisema mchezo ulikuwa mgumu na wanamshukuru Mungu kwa matokeo ambayo walipata katika mchezo huo.

"Tulijitahidi sana, mechi ilikuwa ngumu na matokeo tuliyopata ni sehemu ya mpira," alisema kwa kifupi kiongozi huyo anayesimamia mchakato wa usajili wa wachezaji.

Vikosi vya Simba na Yanga vyote zimesharejea jijini Dar es Salaam kwa ajili ya mapumziko na baada ya muda mfupi watakusanyika kuanza maandalizi ya msimu mpya.

# Nabi: Yanga haikuwa na bahati

**Na Saada Akida, KIGOMA**

BAADA ya kupoteza katika mchezo wa Fainali ya Kombe la Shirikisho la Soka Tanzania, TFF, Kocha Mkuu wa Yanga, Nesreddine Nabi, amesema wachezaji walipambana, lakini bahati haikuwa kwao na kupoteza mchezo huo mbele ya Simba.

Akizungumza na gazeti hili jana, Nabi alisema kwamba baada ya kupoteza fainali hiyo kwa sasa hakuna la kufanya na kufanyia kazi mapungufu yao kwa ajili ya kuimarisha kikosi kwa ajili ya msimu ujao.

Alisema mechi ilikuwa ngumu kwa pande zote mbili na Simba waliingia kivingine na hawakutaka kufungwa kwa mara nyigine.

**"Ninawapongeza Simba kwa kutwaa ubingwa wa FA, pia wachezaji wangu wamepambana ila hatukuwa na bahati huku tukiadhibiwa kwa makosa yetu. Kilicho tokea hatuna cha kufanya, imeshatokea na ili kuwa fainali na kila mtu ameona kwamba, iliku wa ngumu na mwisho wa siku tumepoteza hivyo tunajipanga kwa wakati mwingine," alisema Nabi.**

Alisema sasa wanajipanga kwa ajili ya kufanya maboresho ya kikosi chao kwa kusajili ya wachezaji wapya kulingana na mahitaji aliyopendekeza kwa kukabidhi viongozi kufanyia kazi.

Nabi alisema tayari viongozi wameanza kufanyia kazi mapendekezo hayo na anatarajia kuimarisha kikosi chao kwa msimi ujao endapo viongozi hao walitumia mbinu alizowapa katika usajili.

Alisema mbinu kubwa ni kuhakikisha wanashirikiana vizuri na watu maalum (maskauti) kuangalia wachezaji ambao anawahitaji kwa msimu ujao kwa lengo la kuimarisha kikosi cha timu hiyo.

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >